SUPA JACKPOT
TZS.1,157,290,273
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

# Nipashe

Alhamisi Septemba 28, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581447
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

**WATANZANIA** milioni 7.9 wadaiwa wana maradhi moyo

UKURASA 3



**TANZANIA,** Marekani zafurahia matokeo chanya mpango lishe

UKURASA 3



**MSD** yaongeza ununuzi bidhaa za tiba kutoka viwanda vya ndani

UKURASA 4



Ludovick Utouh

## Pangua pangua ya Rais Samia yamwibua CAG mstaafu Utouh

UKURASA 2

# Mkakati mzito wa TANESCO kukabili makali ya umeme

UKURASA 2



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, na Mkewe Mama Mariam Mwinyi (kushoto), wakipokea zawadi ya mboga za majani kutoka kwa mjasiriamali Asha Abdalla wa Kikundi cha Msonge Organic (kulia), alipotembelea mabanda ya maonyesho, baada ya kufungua Tamasha la Kilimo Hai, katika viwanja vya Kizimbani, mkoa wa Mjini Magharibi jana. **PICHA: IKULU**

## Mwinyi ahimiza kilimo hai kwa afya na utalii

UKURASA 3



Waumini wa dini ya Kiislamu wakiwa katika maandamano ya kumbukumbu ya kuzaliwa kwa Mtume Muhammad (S.A.W), Dar es Salaam juzi jioni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

**MICHEZO** **TANZANIA RASMI MWENYEJI AFCON 2027** UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Pindi Chana (wa pili kulia), akikata utepe kuzindua miongozo ya ulinzi wa mashahidi, usimamizi wa mali zinazopatikana kwa njia ya uhalifu na utakaowasaidia wachunguzi, wapelelezi na waendesha mashtaka katika kushughulikia maombi wanayoyapeleka na kuyapokea kutoka nje ya nchi katika ushirikiano wa kimataifa, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), Sylvester Mwakitalu (wa pili kushoto), Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, CP Salum Hamduni (kushoto) na Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar (DPP), Mgeni Jailani Jecha. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mkakati mzito TANESCO kukabili makali umeme

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Umeme la Tanzania (TANESCO) limeweka wazi mikakati mipya ya kukabiliana na upungufu wa umeme nchini unaochangia kukatika mara kwa mara.

Pia shirika hilo limesema limejipanga kuyapunguza makali yaliyopo ndani ya wiki mbili kuanzia sasa.

Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Gissima Nyamo - Hanga, akizungumza jana na waandishi wa habari kuhusu upungufu wa umeme katika vituo vyake, alisema matarajio ni kuondokana na tatizo hilo ndani ya miezi sita.

"Matarajio yetu hiki kiwango cha upungufu wa megawati 400 tutakuwa tutakipunguza polepole wakati tunayafikia malengo niliyoyaanisha. Tunatarajia ndani ya wiki mbili (kuanzia jana) tatizo hili litaanza kupungua. Mpango tulionao ni wa kuendelea kupunguza kwa wastani wa megawati 100 kwa kila mwezi," alisema.

Alisema wanatarajia hadi mwishoni mwa Machi, mwakani, tatizo hilo liwe limekwisha kwa kuwa watakuwa wamekamilisha matengenezo ambayo yanaendelea kwa mitambo na visima vya gesi asilia.

Upungufu wa umeme, alisema unachangiwa na kiasi kikubwa na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi zinazotumia nishati hiyo, takribani asilimia 12 ikilinganishwa na mwaka jana.

"Upungufu wa maji kwenye vituo vya kufua umeme unatokana na mabadiliko ya tabianchi na kuathiri mabwawa yetu. Kingine ni matengenezo yanayoendelea kwenye visima vya gesi asilia na mitambo ya kuzalisha umeme kwa gesi asilia," alisema.

Nyamo-Hanga alisema kutokana na hali hiyo, baadhi ya maeneo nchini yamekuwa yanakosa huduma ya umeme kwa nyakati tofauti.

Alisema shirika limepokea taarifa na tayari limeanza kutekeleza maagizo yaliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kupitia wizara ya nishati.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, kuna matengenezo katika mtambo wa Ubungo namba moja na mtambo wa gesi Ubungo namba mbili na mtambo wa gesi wa Kinyerezi I. alisema vyote hivyo vimesababisha kuwapo kwa upungufu wa umeme unaokadiriwa kufikia megawati 400.

Alisema tayari jitihada mahususi za utekelezaji za kukabiliana na tatizo hilo zimeanza kwa kuharakisha matengenezo ya mitambo ya kuzalisha umeme na kutengeneza visima vya gesi kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC).

Nyamo-Hanga alisema wanakamilisha ukarabati wa mitambo hiyo kwa haraka zaidi ili ianze uzalishaji, kuharakisha ukarabati wa visima vya gesi ili kuondokana na tatizo la uhaba wa gesi.

"Shirika linaendelea kukamilisha utekelezaji wa Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere litakalokuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 2,115 ambao mpaka sasa umefikia asilimia 92," alisema.

Alisema pindi mradi huo utakapokamilika na kuingizwa kwenye gridi ya taifa utachangia kuimarika kwa hali ya umeme nchini kwa kiasi kikubwa.

Nyamo-Hanga alisema umeme wa Bwawa la Nyerere ukiingia kwenye gridi ya taifa utaendelea kutumika kwa miaka 10 bila taifa kupungukiwa na nishati hiyo.

"Shirika linawashukuru wateja wote na kuwaomba kuwa wavumilivu katika kipindi hiki cha mpito na kwamba, shirika litaendelea kutoa taarifa za upatikanaji wa umeme kwa kadri hali itakavyozidi kuimarika.

"Taarifa hizi zitatolewa kupitia vyombo vya habari mbalimbali, mitandao yetu ya kijamii, tovuti rasmi ya shirika na ofisi zetu zilizopo katika mikoa, wilaya nchini," alisema.

Kuhusu baadhi ya maeneo kukatiwa umeme asubuhi na usiku, aliomba kujua ni wapi ili wataalam washughulikie kwa kuwa utaratibu ni kwamba kama kuna upungufu wakati wa mchana wanatarajia usiku watu wapate huduma.

"Kuna changamoto ya ongezeko la watu kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi. Wanahabari mtusaidie kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira ili kujihakikishia unyeshaji mzuri wa mvua na pia kulinda matumizi muhimu ya maji hasa yanayotumika kwa ajili ya kuzalisha umeme," alisema.

Kuhusu maelekezo ya Rais Samia aliyoyatoa kwake, alisema ameyapokea na tayari ameanza kuyafanyia kazi.

## Pangua pangua ya Samia yamwibua CAG mstaafu uadilifu viongozi wanaoteuliwa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

PANGUA pangua ya viongozi serikalini na taasisi zake inayofanywa mara kwa mara na Rais Samia, imemwibua Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Mstaafu, Ludovick Utouh, huku akitaja mambo kadhaa ya kuzingatia katika kudhibiti ubadhirifu wa fedha za umma.

Katika kufanya hivyo, Utouh amesema watu wanaoteuliwa katika nafasi mbalimbali za uongozi, wachunguzwe ili kujua uadilifu wao kabla ya kupewa nyadhifa za kushika mamilioni ya fedha.

Akihojiwa juzi na kituo cha televisheni cha Azam, Utouh alitaja mambo mengine kuwa ni ni kutekeleza mapendekezo ya CAG, ukaguzi wa ndani madhubuti na usimamizi wa dhati kutoka kwa maofisa mashuhuli kuwasimamia walio chini yao.

Kuhusu kudhibiti ubadhirifu huo, Utouh alisema: "Ni nani hawa wanaoteuliwa kushika hizi nafasi, wawe ni watu wamechunguzwa, wamepekuliwa na kuonekana ni watu wanaofaa na hiki ni kigezo muhimu sana."

Alisema ni vyema kuangalia hao wanaokabidhiwa mamilioni ya fedha kama wana uadilifu wa kutosha.

"Ajira serikalini labda inawalinda sana walioajiriwa na hivyo kuwapa kiburi cha kufanya wakati mwingine vitendo ambavyo havipaswi kufanyika," alisema huku akishauri sheria za ajira ziangaliwe la sivyo itafika mahali pabaya.

Naye mwanasiasa mkongwe, Hamad Rashid Mohamed, alisema: "Unapokwenda kufanya ziara jambo unalolikuta limekaa pale halitatuliwi na mkuu wa mkoa na wilaya upo wewe huwajibiki, tatizo letu ni kuwajibika. Hakuna kuwajibika kwenye utekelezaji wa mambo tunayoyaamua."

Hasmad pia alisema wananchi wapewe taaluma juu ya haki zao ili kuongeza uwajibikaji.

"Bila kufanya hivyo wananchi watakuwa hawajui kwa mfano bajeti imepitishwa halmashauri inapata kiasi fulani mgawano wake ukoje na unatarajia lini zitaanza kufanya kazi wanapaswa waelewe na kufika kwenye vikao halali," alisema huku akitolea mfano nchini Zambia msimamizi wa mradi anaandikwa ili umma ujue.

"Kamati ya bunge ikienda pale si kwamba inambana katibu mkuu bali inambana yule ambaye anasimamia. Nadhani haya yakifanyika kutakuwa na uwajibikaji," alisema.

Mwanasiasa huyo alihimiza kupambana na rushwa ili kuwa na nidhamu.

Mapendekezo hayo yanakuja baada ya ziara ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliyofanya hivi karibuni katika mikoa ya Kigoma na Kagera na kubaini matumizi mabaya ya fedha za miradi ya maendeleo.

# Mwinyi ahimiza kilimo hai kwa afya na utalii

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewataka wadau wa kilimo kuendelea kuliimarisha tamasha la Kilimo Hai liwe kubwa zaidi na endelevu ili kuwavutia watalii.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana alipofungua tamasha la kwanza la Kilimo Hai kwenye viwanja vya Maonyesho ya Kilimo, Kizimbani mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.

Alisema Febuari, mwaka huu, kwenye maadhimisho ya Siku ya Utalii Duniani, serikali ilizindua azimio la utalii endelevu lililoazimia kuitangaza Zanzibar kuwa kivutio cha kijani na kuzitaka hoteli zote za utalii nchini zitumie mazao ya Kilimo Hai na kuweka vyakula vya asili ya Zanzibar.

Pia alisema, azma ya serikali kwa hoteli hizo za kitalii kuona uchakataji wa taka unatengenezewa kuwa malighafi endelevu na kutunza mazingira na kuongeza kuwa serikali haina budi kuendelea kuchukua hatua ya kutimiza asili ya Zanzibar na kuhakikisha watalii wanaoingia Zanzibar wanaendelea kufahamu utamaduni wa Zanzibar.

Dk. Mwinyi pia alipongeza shughuli za uzalishaji na utengenezaji wa vitu vya asili ikiwemo ufinyanzi wa vyungu, kudarizi vikoi, ushonaji kofia za asili, matumizi ya mapakacha na masusu, mikoba ya ukili na mikeka kwa sehemu kubwa vinaendana na sera ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi na kusaidia kukuza uchumi.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na wadau wa sekta hiyo, wamemaliza rasimu ya mikakati ya kilimo hai kwa Zanzibar na kueleza matumaini yake kuwa utekelezaji wake utakuwa suluhisho la changamoto za kilimo hai kinazokabiliana nazo ikiwamo pembejeo za kibaolojia, elimu kwa wakulima na wafugaji na upatikanaji wa masoko ndani na nje ya nchi.

Dk. Mwinyi alisema serikali inafamu fursa zilizomo ndani ya kilimo hai na kwamba dhamira yake iwapo mkakati ulioandaliwa ukatengenezewa programu Madhubuti, utekelezaji utawapa fursa vijana kuanzisha biashara za kutengeneza viuatilifu na mbolea hai kwa kusaidia upatikanaji wa masoko ya ndani na nje ya nchi, hivyo kuitangaza Zanzibar kama kivutio cha kijani.

Kuhusu matumizi ya mbolea za kemikali kwenye utoaji wa elimu kwa watumiaji na walaji, Dk. Mwinyi alisema haja ya kuielimisha jamii kuhusu faida katika kuimarisha lishe ili kusaidia kupunguza maradhi yasiyoambukiza kama shinikizo la damu, kisukari na moyo.

Kadhalika, Rais Mwinyi alisema uhalisia wa tamasha hilo unaonekana pia kwenye shughuli zingine za ujasiriamali.

Waziri wa Kilimo, Shamatta Shaame Khamis, alielezea azma ya wizara hiyo inavyoendeleza jitihada za serikali kushirikiana na taasisi zote za Zanzibar zinazojishughulisha na kilimo kwa ujumla wake na mafaniko yaliyofikiwa.

Alisema serikali pia inatoa huduma kwa wakulima wanaozalisha mazao kwa kutumia mbolea za kemikali na kuwapa elimu ya namna bora ya kutumia pamoja na kuhamasisha jamii namna bora ya kutumia viuatifu kwaajili ya kuendeleza uzalishaji maalumu.

Mwakilishi wa Bububu, Mudrik Ramadhan Soraga alisema fursa za wananchi wa jimbo hilo hasa kwa shehia za Dole na Kizimbani wanavyonufaika na fursa za Kilimo hai na kueleza wanavyojikita kwenye kilimo cha mazao ya viungo na mboga kwa kutumia mbinu bora za kilimo chenye tija kwa afya.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Kilimo Hai Zanzibar (ZOI), Dk. Mwatima Abdala Juma, alisema kuna haja kwa wakulima na jamii kuendelea kukiimarisha kilimo hai ili kuimarisha afya za watu na udongo kwa kuepuka matumizi ya mbolea zenye kemikali.

## Tanzania, Marekani zafurahia matokeo chanya mpango lishe

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI za Marekani na Tanzania zimefurahia matokeo chanya ya mpango wa kuimarisha lishe endelevu katika ngazi ya kaya.

Mpango huo wa miaka mitano uliofadhiliwa na Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) umeleta maendeleo makubwa katika mikoa ya Dodoma, Iringa, Morogoro na Rukwa.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Ofisi ya Kukuza Uchumi ya USAID, Colin Dreizin, lengo kuu la mradi huo lilikuwa kuimarisha juhudi za kuboresha lishe katika ngazi ya kaya kupitia ushirikiano na serikali za mitaa, asasi zisizo za kiserikali na zaidi ya mashirika 300 ya sekta binafsi.

Alisema mradi huo umesaidia kuhimiza uzalishaji na upatikanaji wa vyakula vya aina mbalimbali kwa kaya, hivyo kuboresha afya katika ngazi hiyo kwenye mikoa iliyokuwa ikitekeleza.

"Tangu kuanzishwa mwaka 2018, Mradi wa Lishe Endelevu ulitoa dola za Marekani milioni 25 na kuhakikisha zaidi ya wanawake milioni 1.6 na watoto milioni 1.2 katika mikoa ya Dodoma, Iringa, Morogoro na Rukwa wanapata huduma muhimu za lishe.

"Katika kipindi hicho, USAID ilifanya kazi kwa karibu na Wizara ya Afya ya Tanzania, Ofisi ya Rais TAMISEMI, na wadau muhimu kama vile Deloitte, AAPH, TMG, na PANITA," alisema.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohammed Mchengerwa, alisema mpango huo ulisaidia kusimamia uendelevu wa kilimo mseto na ufugaji, hivyo kuongeza upatikanaji wa chakula chenye lishe bora.

"Tunaishukuru sana USAID kwa kuimarisha eneo la lishe nchini Tanzania. Leo (jana) tumeona mafanikio ya miaka mitano ya mradi wa USAID Lishe Endelevu kupitia kitabu kilichoangazia mikoa hiyo minne," alisema Mchengerwa.




Wachuuzi wakiwa wamepanga bidhaa zao kwenye eneo la kusimama abiria katika kituo cha daladala cha Makumbusho, Dar es Salaam jana na kusababisha usumbufu mkubwa kwa abiria. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Watanzania milioni 7.9 wanaugua maradhi ya moyo

**Na Christina Mwakangale**

WATANZANIA 7,930,000 wanasumbuliwa na magonjwa ya moyo ambayo kwa kiwango kikubwa huchangiwa na lehemu kwenye mishipa ya damu.

Watu hao wanakadiriwa kuwa sawa na asilimia 13 ya Watanzania wote huku ikibainishwa kuwa wanaougua kisukari ndio wako hatarini mara tano zaidi kupata maradhi hayo kulinganishwa na makundi mengine.

Rais wa Chama cha Madaktari Bingwa wa Moyo Tanzania (THF), Dk. Robert Mvungi, aliyasema hayo jana akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam kuelekea Siku ya Moyo Duniani itakayoadhimishwa kesho. Maadhimisho hayo yameandaliwa na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) kwa kushirikiana na THF.

Alisema maadhimisho ya mwaka huu yenye kaulimbiu 'Tumia Moyo Kulinda Moyo Wako' yatafanyika kwa kufanya upimaji wa bure wa magonjwa ya moyo na yatafanyika kesho na keshokutwa katika Hospitali ya Dar Group - JKCI.

"Nchi yetu imepiga hatua kubwa katika kupambana na kutibu magonjwa ya moyo ndiyo maana chama kimeona ni heri kuipandisha hadhi JKCI kutokana na kutibu, kukinga magonjwa ya moyo na chama tunaandaa maadhimisho haya kwa kushirikiana nao.

"Kutakuwa na kambi ya uchunguzi ili kubaini viashiria au dalili za magonjwa ya moyo. Watu wote wa Dar es Salaam na maeneo jirani wafike na kutambua afya zao. Tunaalika klabu za 'jogging' hasa kutoka wilaya ya Temeke ambako kambi itafanyika ni matembezi ya afya na ya moyo," alisema Dk. Mvungi.

Alisema maadhimisho hayo yalianza tangu mwaka 2000 kwa lengo la kuhamasisha umma kuhusu magonjwa ya moyo ambayo hutokana na athari za kutodhibitiwa mfumo wa utendaji kazi wa damu kama vile kuziba kwa mishipa ya moyo ambayo ikiathirika inaweza kusababisha kisukari.

"Lehemu na mishipa ya moyo ikiziba inaweza kusababisha mshtuko wa moyo na vilevile mishipa ya moyo ikiathirika inaweza kuziba ya kwenye ubongo na hata kutokea kwa kiharusi, hivyo presha ikiwa nayo ni vyema ukaitibu ili isisababishe ugonjwa wa moyo.

"Utafiti tulio nao hadi sasa mtu mwenye kisukari ana uwezekano wa kupata magonjwa ya moyo mara tano zaidi kuliko mtu mwingine. Magonjwa ya moyo ni mzunguko wa vitu vyote vinavyozunguka kuendesha moyo," alisema. Aliongeza kwamba duniani watu milioni 20 hufariki dunia kutokana na kwa matatizo ya moyo, ambayo kwa asilimia 80 ya magonjwa hayo yangeweza kukingika, iwapo ungefuatwa ushauri wa kitalaamu.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, alisema taasisi hiyo inashirikiana na THF ili kutoa nafasi kwa wananchi kufanyiwa uchunguzi na madaktari bingwa wa moyo.

"Serikali imejikita katika kuimarisha sekta ya afya hasa matibabu ya moyo na kuna madaktari bingwa wa moyo. Magonjwa haya ya moyo huchangia vifo vingi duniani na unapokuja mapema ni rahisi kupata matibabu na kupunguza athari.

"Tunalenga kuhamasisha jamii umuhimu wa kulinda afya ya moyo na ni kitu muhimu sana ni vizuri kufanya mazoezi, kwa sababu yanasaidia kukinga magonjwa hayo. Tunatoa elimu kuhusu namna ya kuzingatia lishe na tuanatarajia mgeni rasmi siku ya maadhimisho kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam," alisema Dk. Kisenge.

Kaimu Mkurugenzi wa JKCI Dar Group, Dk. Tulizo Shemu, alisema maadhimisho hayo yanalenga kuleta uelewa kwenye jamii kupunguza idadi ya wanaougua, huku akisema kwamba matibabu ya moyo ni ghali hivyo ili kuzuia ni vyema wananchi wakafanya uchunguzi wa mapema.

# MSD yaongeza ununuzi vifaa tiba katika viwanda vya ndani

**Na Jenifer Gilla**

BOHARI ya Dawa (MSD) imeongeza ununuzi wa bidhaa za afya kwa wazalishaji wa ndani kutoka Sh. bilioni 14.1 mwaka 2021/22 hadi Sh. 39.77 mwaka 2022/23 ili kuvisaidia viwanda hivyo kukua na kupunguza gharama za kuagiza bidhaa hizo nje ya nchi.

Pia imeimarisha mfumo wa usambazaji wa bidhaa za afya kutoka mara nne hadi mara sita kwa mwaka katika kipindi hicho, hivyo kupunguza muda wa vituo vya afya kusubiri bidhaa hizo hali inayochangia kuboresha huduma ya afya.

Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Mavere Tukai, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, alipozungumza na wahariri wa vyombo vya habari. Alisema MSD inatumia wadau wa nje na ndani ya nchi kuongeza uzalishaji wa bidhaa za afya nchini.

Alisema taasisi hiyo iliamua kuviunga mkono viwanda hivyo ili kuviongezea nguvu visife kwa kuwa vinatumia gharama kubwa katika uzalishaji pia kutomwathiri mteja ambaye ni hospitali kununua bidhaa hizo kwa bei ya juu tofauti na iliyoko sokoni.

Pia alisema walianzisha zabuni maalum zinazohusu wazalishaji wa ndani na kuongeza mikataba ya muda mrefu ya bidhaa za afya kutoka 100 yenye bidhaa 711 mwaka wa fedha 2021/22 hadi mikataba 233 yenye bidhaa 2,209 kwa mwaka 2022/2023 ili kuvipa kipaumbele viwanda hivyo.

Ili kuboresha huduma za usafirishaji wa bidhaa zao, Tukai alisema bohari ilinunua matrela 16 ya kusambaza bidhaa za afya yaliyogharimu Sh. bilioni 2.6 na kuongeza kasi ya usambazaji kutoka bidhaa za Sh. bilioni 320 kwa mwaka wa fedha 2021/22 hadi Sh. bilioni 373 kwa mwaka 2022/23.

Pia alisema wamebadilisha mfumo wa utoaji huduma na sasa wamehamia kwenye Teknolojia ya Mawasiliano (TEHAMA) ili kuhakikisha bidhaa hizo zinapokelewa kieletroniki katika vituo vya kutolea huduma na kurahisisha ufuatiliaji wa magari ya kutolea huduma hiyo.

Mkurugenzi huyo alisema bado bohari hiyo inaendelea kufanya maboresho ili kufikia malengo ya tiba na sasa mikakati iliyopo ni pamoja na kuimarisha uhifadhi wa bidhaa za afya kwa kujenga maghala ya kisasa katika mikoa ya Dar es Salaam, Kagera na Mwanza.

Aliitaja mikakati mingine kuwa ni kuimarisha mifumo ya usimamizi wa utendaji wa taasisi, kugatua shughuli zilizokuwa zinafanyika makao makuu kwenda ofisi za kanda na kutumia vyanzo mbadala vya fedha ili kuiongezea taasisi uwezo.

"Pia tunaboresha ushirikiano na kuongeza ushawishi katika ngazi ya sekretariet ya (Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika) SADC na katika ngazi ya nchi za ukanda huo kupitia balozi zetu," alisema Tukai.

Mwenyekiti wa Jukwa la Wahariri Tanzania (TAF), Deodatus Balile, alilipongeza bohari hiyo kwa kuendelea kufanya kazi ya kupeleka huduma ya afya kwa jamii bila kujali hali yao ya kiuchumi.

Alitolea mfano kuwa mwaka 2019 bohari hiyo ilikuwa na bajeti sifuri kutoka serikalini lakini ilitafuta vyanzo vyake vya fedha kuhakikisha kuwa kazi ya kuitumikia jamii kupitia afya inaendelea kuwapo.

Pia aliishauri kuomba sheria inayowasimamia ibadilishwe ili wawe kuanzisha mfuko endelevu, fedha zinazokushanywa kupitia kampuni tanzu zihifadhiwe katika mfuko huo ili hata ikitokea wakakosa fungu serikalini wawe tayari na fedha za kujiendesha.




Mkurugenzi Mtendaji wa Bohari ya Dawa (MSD), Mavere Tukai (kushoto), akizungumza katika mkutano na wahariri wa vyombo vya habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akitoa taarifa ya utendaji, mafanikio na mwelekeo wa bohari hiyo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TAMWA: Rushwa ya ngono vyuoni inaathiri wanafunzi

**Na Beatrice Moses**

RUSHWA ya ngono inayodaiwa kuhusisha baadhi ya wahadhiri kwenye vyuo vikuu na vya kati imetajwa kusababisha athari kadhaa kwenye jamii, ikiwamo hofu kwa baadhi ya wazazi na wanafunzi watarajiwa kujiunga na vyuo hivyo.

Vile vile, kwa vyombo vya habari hasa waandishi wa habari wa kike walio kwenye mafunzo inakwamisha umahiri wao wa uandishi na kusababisha wengine kuvunjika moyo na kuikimbia fani hiyo.

Hayo yamebainishwa jana, jijini Dar es Salaam, kwenye warsha iliyoandaliwa kwa wanahabari wanawake, iliyoandaliwa na Chama cha Waandishi Wahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), kwa ufadhili wa Mfuko wa Women Fund (WFT).

Mkuu wa Dawati la Elimu kwa Umma wa Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Kinondoni, Bibie Msumi, alisema taarifa za malalamiko kuhusu rushwa ya ngono walizozipokea, nyingi zilihusisha wahadhiri, hali ambayo pia inasababisha kuharibika kwa sifa ya chuo kwa baadhi ya wanajamii.

"Miongoni mwao wawili wameshtakiwa mahakamani, zipo taarifa nyingine kadhaa tulipata changamoto wanafunzi husika walisita kutoa ushirikiano wa kufanikisha kuwanasa watuhumiwa husika, ipo nyingine mhadhiri husika aliacha kazi ghafla baada ya kukutwa akiwa kwenye mazingira yenye utata na mwanafunzi aliyekamatwa akiangalizia mtihani," alisema Msemi ambaye pia ni Mwendesha Mashtakta wa TAKUKURU.

Akizungumzia kuhusu rushwa ya ngono kwenye maeneo ya kazi, Msumi alisema, kunapaswa kuwa na kamati/ dawati la maadili ofisini ambalo linapaswa kuandika taarifa ya hali ilivyo kila baada ya miezi mitatu, kuwaisilisha TAKUKURU kwa hatua nyingine, kisha taarifa ya ujumla hupelekwa kwa Katibu Kiongozi kwa ufuatiliaji zaidi.

Mkurugenzi wa TAMWA, Dk. Rose Reuben, alisema utafiti uliofanywa mwaka 2021 ulibaini kuwa asilimia 68 ya wanawake walioathiriwa na rushwa ya ngono wakiwamo waandishi wa habari wanawake hawakuwa tayari kuzungumza kutokana na kuhofia kudhalilika zaidi au kupoteza ajira.

"Katika utafiti tulioufanya vyuo vikuu, wahadhiri wengi walituambia kuwa wanafunzi wenyewe wanajipeleka kwao, wakati kwenye vyombo vya habari wanahabari wanafunzi wa kike wamekuwa wakiwekwa kwenye wakati mgumu na baadhi ya wahariri wanaume wakikusudia kuwanasa kwa ngono," alisema.

Mwenyekiti mstaafu wa Tamwa, Dk Ananilea Nkya, alisema mwandishi wa habari wa kike anaweza kupambana na rushwa ya ngono kwa umakini kwa kujituma kufanya kazi kwa bidii, badala ya kutegemea upendeleo.

"Binafsi nimewahi kuombwa rushwa ya ngono, nilipokataa huyo mhariri aliminya mwaliko wangu wa safari ya kikazi ya nje ya nchi, nilipobaini sikuvunjika moyo, niliendelea kufanya kazi kwa bidii, ilionekana hatimaye nikapewa cheo cha kuwa mhariri," alisema Nkya.

# 'Wenye nafasi za uongozi, hawajui kuongoza'

**Na Beatrice Shayo**

TAASISI ya Uongozi nchini imetoa ripoti ya utafiti uliofanywa na Chuo Kikuu cha Havard cha nchini Marekani, ambao unaonyesha watu wengi duniani wana nafasi za uongozi, lakini hawajui kuongoza.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi hiyo, Kadari Singo, alitoa taarifa ya utafiti huo wakati akitia saini makubaliano na Jeshi la Polisi, kuanza kuitumia maktaba ya Taasisi ya Uongozi kujifunza mambo mbalimbali.

Taasisi hiyo inashirikiana na Chuo Kikuu cha Havard na Chuo Kikuu cha Oxford.

Alisema bado kuna changamoto ya kuwajenga viongozi hali inayosababisha wakipewa nafasi kushindwa kuongoza licha ya kuzitaka nafasi hizo.

Akifafanua tofauti kati ya kuwa na nafasi ya uongozi na kuwa kiongozi, alisema ripoti ya utafiti uliofanywa na Chuo Kikuu cha Harvad unaonyesha watu wengi duniani wana nafasi za uongozi, lakini hawaongozi.

"Watu wanazishikilia hizo nafasi, wanazigombea na wanazing'ang'ania kweli kweli, akishika haongozi, unakuta watu wanajiongoza wenyewe na kusambaratika sababu kubwa hatujengi viongozi, tunawachukua na kuwaweka tunafanya kama tunajaribisha vile...," alisema Singo.

Amesema viongozi duniani ni lazima wajengwe, kuna watu ambao wamezaliwa kuongoza. "Hii nilisikia kwa wagombea ubunge maeneo ya vijijini, kuna wazee ambao wakitaka uwe mbunge utakuwa na asipotaka haushindi. Huyu hajawahi kuingia darasani, lakini anaheshimika kijijini na neno lake akisema safari hii tunampigia fulani kura, anasikilizwa."

Ameshauri viongozi kujengwa kwa njia mbalimbali moja wapo ni kufanya utafiti ambao utamsaidia kiongozi kuwa na taarifa, kuingia darasani na kusoma vitabu.

"Utafiti unaonyesha watu wengi waliofanikiwa duniani walikuwa ni wasomi wazuri wa vitabu, hivyo ni muhimu kuzingatia usomaji wa vitabu."

Aidha, alisema Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) amependekeza jeshi hilo lianze kuwa la kisasa kwa kuanza kutumia maktaba ili kujifunza zaidi dunia inakoelekea.

Lengo la Taasisi hiyo ni kuwafanya viongozi waliopo serikalini, sekta binafsi na asasi za kiraia wapate fursa ya kujiendeleza kwa kuwa vitabu hivyo vimeandikwa na watu wenye uwezo mkubwa.

"Kiongozi anapopata fursa ya kupata vitabu na kujisomea anajiongezea maarifa lengo la taasisi hii ni kushirikiana na taasisi mbalimbali likiwamo jeshi la polisi wanufaike na makataba yetu ambayo tunashirikiana na Chuo Kikuu cha Havard na Oxford wanatupatia fursa ya majarida na machapisho mengi," alisisitiza.

Alisema kiongozi anapofanya maamuzi ni lazima afanye utafiti kwa njia ya vitabu ili uweze kumsaidia kutoa wenye maarifa ndani yake.

# Wasiojulikana wafanya mauaji ya kikatili

**Na Elizabeth Zaya**

WATU wasiojulikana wanadaiwa kufanya mauaji ya kikatili kwa kumbaka na kumnyonga binti mwenye umri wa miaka 21, mkazi wa Malamba Mawili, wilayani Ubungo, Dar es Salaam.

Tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia juzi, njia panda maarufu kwa TMK.

Akisimulia tukio hilo, baba wa binti huyo (jina tunalihifadhi), alisema mwanawe alikutwa na tukio hilo la kutisha usiku wa saa tano alipokuwa akirejea nyumbani akitokea kazini kwake Sinza.

Alisema kabla ya kutoka kazini aliwasiliana na mdogo wake ambaye alimwagiza amnunulie matunda na kumpelekea nyumbani.

"Kabla hajatoka kazini kwake mdogo wake alimpigia simu na kumwomba amnunulie matunda amletee nyumbani, alipofika Mbezi alimpigia mdogo wake kumwambia tayari amemnunulia matunda kama alivyotaka," alisimulia baba huyo.

Alisimulia kuwa, alimwambia mdogo wake kuwa amepanda bajaji na anaelekea nyumbani na atafika muda si mrefu.

"Bajaji aliyopanda ni zile za kuchangia zinazokuja Malamba Mawili, na alipofika kituo cha nyumbani kinachojulikana kama TMK akampigia tena mdogo wake kwamba tayari ameshuka, lakini cha kushangaza mpaka dakika 10 tangu alipomwambia ameshuka kituoni hakufika nyumbani," anasimulia.

"Mdogo wake alivyoona vile akapiga tena simu, lakini haikupatikana na kwa kuwa yeye ni mwanafunzi akaona kwamba huenda dada yake kuna mahali kapitia, labda simu yake imezima, akaamua kwenda kulala ili asichelewe shuleni siku inayofuata.

"Hawa mabinti zangu huwa wanalala vyumba tofauti, kwa hiyo huyu mdogo alijua tu atachukua matunda yake hata kesho yake asubuhi, lakini cha kushangaza hata alivyoamka hakumuona dada yake akajua atakuwa ameondoka kwenye shughuli zake na yeye akatoka nyumbani kwenda shuleni muda wa saa 12 asubuhi."

Baba huyo aliendelea kusimulia kuwa alipofika barabarani kwenda kutafuta usafiri wa kuelekea shuleni alikuta kundi la watu pembezoni mwa barabara wakiwa wanashangaa huku wakizungumza kwamba kuna binti amefariki.

"Binti yangu alisogea na kumtambua dada yake akiwa ndiye aliyelazwa pale na nguo zake wamemvua wakaziweka pembeni halafu mguu wake mmoja umekunjwa na kukandamizwa mgongoni, na ndipo tukapewa taarifa kwenda kumtambua," anasimulia baba mzazi huyo.

"Polisi walipewa taarifa na wakaja kuchukua mwili kuufanyia uchunguzi na matokeo ya uchunguzi ni kwamba alibakwa, akavunjwa nyonga na wakamnyonga na wakaturuhusu tuchukue tukazike kwa kuwa umeharibika sana na wao wanaendelea na kutafuta wahalifu wa kitendo hicho."

Alisema jana walisafirisha mwili kuelekea Machame, mkoani Kilimanjaro kwa ajili ya maziko.

Hata hivyo, juhudi za Nipashe kumpata Kamanda wa Polisi Kinondoni kuthibitisha tukio hilo, hazikuzaa matunda.



Mkuu wa Polisi wilaya ya Muheza, mkoani Tanga , Hadija Sokolo (kushoto), akitoa maelekezo kwa askari wa kike eneo la Mvuleni juzi, kabla ya kuanza safari ya kwenda Korogwe katika kongamano la Ongea Nao linalolenga kupinga ukatili wa kijinsia kwa watoto na wanawake na kuelimisha jamii kuhusu ulinzi na usalama. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Bosi mpya CMA aainisha mikakati utatuzi migogoro

**Na Halfani Chusi**

MKURUGENZI wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi Tanzania (CMA), Usekelege Mpulla, ameainisha mipango ya kumaliza migororo ya kazi ndani ya siku 21.

Amesema katika kufanya hivyo, lengo ni kuweka mazingira ya wafanyakazi na waajiri kutumia muda mwingi katika kuzalisha badala ya kutatua matatizo.

Mkurugenzi huyo aliyasema hayo jana, baada ya kuapishwa na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi, Dk. Yose Mlyambina, katika hafla fupi iliyofanyika Dar es Salaam.

Kabla ya uteuzi huo alikuwa Mwamuzi Mwandamizi na Ofisa Mfawidhi wa CMA Kanda ya Dar es Salaam.

Mteule huyo alisema kwa sasa wameweka mkakati madhubuti wa kumaliza migogoro inayohusu wafanyakazi na waajiri ndani ya siku 21.

"Kipaumbele chetu migogoro iishe ndani ya wakati na kwa njia ya usuluhishi. Lakini tutaendelea kutoa elimu ya namna bora ya kumaliza migogoro kwa njia ya kuweka mabango, kutoa semina na kutumia vyombo vya habari.

"Pamoja na majukumu ambayo nimeapa wananchi wanachotarajia ni ufanisi chini ya uongozi wangu, matarajio yangu ni kuleta ufanisi zaidi ili kukidhi matarajio ya wengi na kutatua migogoro kwa wakati," alisema.

Mpulla alisema kesi inapocheleweshwa inamuumiza mtumishi ashindwe kufaidi mazuri ya kazi, na kwamba anataka kuwe na tume ya usuluhishi inayowafuata wafanyakazi huko waliko kwenda kusuluhisha migogoro yao.

Awali, Dk. Lyambina alimsihi mteule huyo kufanya kazi kwa bidii kwa kufanikisha majukumu ya tume hiyo ili kufikia lengo la serikali.

Alisema anapaswa kutambua kwamba ameteuliwa kubeba jukumu kubwa kwa kuongeza ufanisi na kuleta mbinu chanya katika kutatua migogoro ya watumishi.

"Ngoja nikumbuke maneno ya Mwalimu (Julius) Nyerere katika hotuba yake aliyoitoa mwaka 1962 alisema: 'hatuwezi kutatua matatizo yetu kwa kujidanganya kuwa hayapo.'

"Mwamuzi au mtu mwenye mamlaka ya kuamua anatakiwa kufanya kazi kwa mujibu wa sheria na kama kifungu hicho hakitakuwapo anapaswa kuamua kwa mujibu wa sheria na utamaduni wa jamii husika.

"Ni jukumu letu kwa pamoja, kutumikia jamii ya Watanzania kwa uaminifu mkubwa. Tunatazamia majalada yatawasilishwa mahakama kuu kwa wakati na taasisi hii itakuwa kisima cha ubunifu kwa kufanya mambo yatakayo rahisisha utendaji kazi kwa maslahi ya taifa" alisema Dk. Lyambina.


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya Benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| TEGETA | LUCAS NTIRUHUNGWA MZYENGE | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JAPHET YONA MZAVA | KIGAMBONI | 13/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | ANGWA CONSTRUCTION CO. LTD | NYUMBA | JASSON ALPHONCE MWAKITWANGE | BUNJU 'A' | 10/10/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TANDALE | OSCAR JOSSEY MUNIS | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | VERAELI ELIYA KOMBE | MWANANYAMALA -KINONDONI | 29/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURU | JOSTER JACKSON NSASHE | NYUMBA | KERAMBO CHOGO KERAMBO AND JOASTER | KITUNDA MZINGA | 17/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURU | MHINA JOSEPH KWELLA | NYUMBA | MHINA JOSEPH KWELLA | PUGU | 17/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | FELIX MAVIKE MSIGWA | NYUMBA | FELIX MAVIKE MSIGWA | ILEMI-MBEYA | 12/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | ANDERSON MITAMBO SANGA | NYUMBA | FELISTER MAMBOLEO | ILOMBA MBEYA | 13/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | YESAYA SAMWEL KIBONDE | NYUMBA | YESAYA SAMWEL KIBONDE | TEMBELA MBEYA | 17/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | NWAKA BENI MWAKAPALILA | 1.NYUMBA 2.KIWANJA | NWAKA BENI MWAKAPALILA | VETA - ISYESYE | 18/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja , Shamba au Gari ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0745707008/0787129539/0714939933**
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote

217620402

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Agizo la Rais kuondoa kero kukatika umeme lifanyiwe kazi

**JUZI** wakati Rais Samia Suluhu Hassan akiwaapisha viongozi aliuowateua kushika nyadhifa mbalimbali, aliwataka wakatekeleze majukumu waliyopangiwa ili wananchi waweze kuhudumiwa bila kuwa na malalamiko.

Viongozi walioteuliwa ni pamoja na bosi mpya wa Shirika la Umeme Nchini (Tanesco), ambaye amepewa miezi sita, kumaliza changamoto ya kukatika kwa umeme katika mikoa mingi nchini.

Nishati ya umeme na maji ni huduma muhimu kwa taifa katika uzalishaji wa viwandani na nyumbani, inapokosekana lazima kutakuwa na malalamiko.

Wafanyabiashara wakubwa na wadogo, wanategemea nishati hiyo katika uzalishaji wa bidhaa zao ili ziweze kuingia sokoni, hivyo inapokosekana husababisha lawama.

Nishati hiyo inapotegemea njia moja pekee ya uzalishaji, ambayo kutokana na mabadiliko ya tabianchi, uhakika wa kupata maji kwa kiwango kinachotegemewa siyo mkubwa ni lazima kuwapo na ubunifu wa kutafuta njia nyingine kukabiliana na hali hiyo.

Wakati Rais akimwapisha bosi mpya wa Tanesco, aliagiza pale alipoishia bosi wa zamani, bosi mpya akaendeleze ikiwamo kufanya marekebisho ya mitambo ya kuzalisha umeme ambayo hayakufanywa kwa muda mrefu ili kuondoa kelele za kukatika kwa umeme kutoka kwa wananchi.

Kwa sasa nchi imeingia kwenye mgawo wa umeme kutokana na kilichoelezwa kuwapo kwa upungufu wa maji kwenye vyanzo vya uzalishaji. Rais alimpa kibarua hicho bosi mpya wa Tanesco na kusisitiza baada ya miezi sita hataki kusikia kelele za kukatika kwa umeme.

Kazi ya kuhudumia wananchi inahitaji ushirikiano mkubwa kuanzia kwa bosi wa juu hadi wafanyakazi wa chini. Na kunapokuwapo na ushirikiano huo wa mawazo, michango na maoni husaidia kuleta ubunifu wa kuboresha utoaji huduma. Mara kwa mara tatizo la kukatika kwa umeme linapoibuka, ndipo hufikiriwa njia mbadala ya uzalishaji wa nishati hiyo badala ya kutegemea uzalishaji kwa njia ya maji pekee.

Hata hivyo, hali ya mvua inapokuwa ya kujitosheleza mawazo yaliyopendekezwa inaonekana yanawekwa pembeni na kusahauliwa kabisa.

Matokeo ya kusubiri uzalishaji wa njia ya maji, ndio hayo husababisha wakati wa ukame vyanzo vinapokuwa na upungufu wa maji, kukwamisha utoaji wa huduma hiyo.

Kuna wakati ilipendekezwa njia mbadala ya kuzalisha umeme kwa kutumia upepo ambayo ingesaidia kupunguza tatizo la upatikanaji wa umeme kama kutakuwa na upungufu wa mvua.

Njia nyingine zinazotumika kama mbadala wa kutegemea umeme unaozalishwa na maji ni wa kutumia sola (umeme unaozalishwa kwa jua). Umeme huu umeokoa wananchi wengi hasa wa vijijini baada ya wengi wao kutumia kuwashia taa na matumizi mengine madogo yasiyohitaji umeme mwingi. Kuna njia nyingine ya kutumia umeme wa jenereta, ambayo gharama yake ni kubwa kwa sababu ni lazima mafuta yatumike kujaza kwenye chombo hicho ili kiweze kutoa huduma hiyo na umeme huo hufanya kazi ya uzalishaji mpaka viwandani.


Kwa watu wenye vipato vya chini njia hiyo hawawezi kumudu na hivyo hukimbilia kwenye umeme wa jua ambao umekuwa mkombozi wa wengi.

Bilashaka, muda aliopewa bosi mpya wa Tanesco utaleta tija katika kupata suluhisho la kuondokana na kero ya kukatika umeme mara kwa mara.

Tanzania imetangaza fursa nyingi za uwekezaji, kama hakutakuwa na umeme wa uhakika wawekezaji wataogopa kuwekeza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Umefika wakati kupatikane mwarobaini kudhibiti mauaji ya 'wivu wa mapenzi'

Na Mary Seme

**KATIKA** miaka ya hivi karibuni imekuwa ni kawaida kusikia watu wakiuana kwa kile kinachoitwa 'wivu wa mapenzi' Kuna simulizi ya hivi karibuni tu huko mkoani Dodoma baada ya dada mmoja aliyekuwa mfanyabiashara wa juisi, aliyekuwa amepanga chumba amedaiwa kuuawa kwa kuchomwa kisu na mpenzi wake wakiwa chumbani.

Dada huyo inadaiwa alikutwa na mauti kutokana na kuwapo kwa ugomvi baina yake na mpenzi wake kwa sababu iliyoelezwa na polisi kuwa huo ni wivu wa mapenzi. Mkasa wa mwanamke huyo na mpenzi wake, ni mojawapo tu ya wapenzi walioingia katika mikasa ya aina hiyo iliyoangukia kwenye mauaji.

Sio ishara nzuri. Ni vyema hatua zikachukuliwa ikiwamo kutolewa elimu ya mahusiano kwa vijana kutoka kwa wazazi, viongozi wa dini na hata wadau mbalimbali na kupitia taasisi mbalimbali ikiwamo katika vyuo, ili kupunguza kama siyo kuondoa kabisa zimwi hili la mauaji yatokanayo na wivu wa mapenzi ambalo sasa linaelekea kuzoeleka hapa nchini.

Watu wafundishwe kuwa mapenzi siyo ajira kama ambavyo wengine wamekuwa wanafanya. Siku hizi imekuwa ni kawaida kwa wadada kueleza shida zao nyingi kwa wapenzi wao, ikiwamo kupewa vitu mbalimbali vya thamani ambavyo pengine si mahitaji ya lazima sana.Wenyewe wakiona ndiyo kupatia maisha lakini kumbe ni kujitengenezea tatizo la baadaye.

Unaweza kuona mwanamke ana maisha mazuri, gari zuri, simu ya gharama, nywele za bei ghali kumbe vyote ni hela anazochuma kutoka kwa wapenzi wake mbalimbali pasina kujua kuwa vitu hivyo vitakuja kumgharimu baadae.

Si vibaya kwa mwanaume kumpa fedha ama vitu vingine vya thamani mwanamke ambaye ana uhusiano naye, lakini ni vyema kujiridhisha ya kwamba mtu huyo anampenda kweli na kwamba hatimaye watafikia malengo.

Kwa upande wa mwanaume, ni vyema kuzingatia kwamba mwanamke unayemhudumia basi una uhakika naye ya kwamba hatimaye mtafunga pingu za maisha, ili usiingie katika mtanziko pale utakapobaini kuwa kumbe mwanamke uliyekuwa ukimhudumia naye ana mpenzi wake, jambo ambalo limechangia wengi kujikuta katika matatizo.

Vipo visa vya watu kudiriki kuwasomesha vyuo wapenzi wao, bila hata ya kutambulika nyumbani kwao na baada ya binti kumaliza kusoma, au akiwa katika masomo anapata mwanaume mwingine huko huko masomoni na kumsahau huyu aliyemsomesha .

Mwanaume ambaye amepambana kulipa ada na michango mingine yote ya chuo katika kipindi chote, binti awapo chuoni akiona hivyo, lazima apate mshtuko na pengine kufanya uamuzi wa kushangaza ingawa kikawaida mchumba hasomeshwi.

Ni makosa kumsomesha na siyo tu kusomesha bali pia, hata kumhudumia mwanamke ambaye hamjaoana kwa kumpa vitu vya thamani kwa kutegemea tu kulipwa kwa kuwapo uhusiano usio rasmi kwa kuwa kazi yako haitatambuliwa na yeyote na kilio chako cha ama kusalitiwa au kukataliwa baadae kitakuwa ni cha kujitakia.

Ni muhimu ukatafutwa muarobaini wa kulimaliza tatizo hili ,vinginevyo tutaendelea kusikia matukio kama haya ya mauaji kwa jina la 'wivu wa mapenzi' yakiota mizizi katika jamii yetu, huku yakiwaacha ndugu jamaa na marafiki katika simanzi na mzigo wa kulea watoto waliotokana na wazazi walioamua kuuana.

Si vibaya katika vyuo vyetu ambako ndiko waliko vijana wengi, pia yapo matukio ya aina hiyo, kukawapo somo la uhusiano na namna ya kukabili changamoto zake. Pia, katika taasisi za dini kama makanisa na misikiti,kuna kila sababu za kuwekezwa elimu hiyo.

## HABARI KITAIFA

# Ushirikiano wa Tanzania, China waleta mafanikio katika biashara, uwekezaji

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, amesema ushirikiano wa miaka 60 kati ya Tanzania na China umeleta mafanikio mengi hususani biashara na uwekezaji.

Makamba amesema Tanzania inajivunia ushirikiano huo ambao umesaidia kuongeza ukuaji wa uchumi, uwekezaji pamoja na kupanua sekta ya utalii.

Aliyasema hayo juzi Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya miaka 74 ya uhuru wa Jamhuri ya Watu wa China.

Maadhimisho hayo yalihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa kitaifa wakiwamo Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye; Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yussuf Masauni, Waziri Mkuu Mstaafu Mizengo Pinda, na mabalozi mbalimbali.

"Tanzania inajivunia ushirikiano wa miaka 60 na China. Tunajivunia uhusiano wa muda mrefu na kwa miaka yote hiyo, mafanikio ni mengi katika nyanja za kimataifa. Kila mwaka uhusiano unaimarika hususani katika biashara na uwekezaji," alisema January.

Alisema China inaongoza kwa kuleta mitaji nchini na inaongoza kwenye ukubwa wa uwekezaji wa kibiashara pamoja na utalii.

"Ni taifa lililotoka katika umaskini hadi kuwa kubwa duniani katika teknolijia, kiuchumi duniani. Mfano huu unatuhamasisha sisi Watanzania," alisema Makamba.

Kadhalika, alisema China ilianzisha mpango mkubwa wa uwekezaji duniani na hadi sasa umetimiza miaka 10, kwamba umekuwa na manufaa makubwa hapa nchini.

Balozi wa China nchini Tanzania, Chen Mingjian, alisema kwa miaka 74 ya uhuru, China imepiga hatua kubwa katika maendeleo ya kiuchumi.

Alisema pato la taifa la China linakua kwa asilimia 5.5 kwa mwaka katika kipindi cha nusu mwaka ya mwaka 2023 na kufikia Dola za Marekani trilioni 8.24.

Pia alisema uagizaji na uingizaji wa bidhaa umeongezeka hadi kufikia Dola za Marekani trilioni 2.8 kwa mara ya kwanza.

Balozi Mingjian alisema uuzaji wa magari katika kipindi cha miezi saba umefikia Dola za Marekani milioni 2.5 na kuifanya China kuwa taifa kubwa duniani katika uuzaji wa magari.

Alisema Shirika la Fedha Duniani (IMF) limetabiri kwamba China itachangia asilimia 34.9 katika uchumi wa dunia.



Baadhi ya wajumbe wa bodi na kamati za elimu, afya na kilimo, kutoka mikoa mbalimbali, wakiwa katika vikundi vya kujadili na kuainisha changamoto kwenye bodi na kamati hizo, katika warsha ya siku tatu ya kuwezesha majadiliano ya uchechemuzi iliyondaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Mabibo Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mfumo mpya kuwaondoa matapeli uwekezaji

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amezindua mfumo wa kielektroniki utakaohudumia wawekezaji sehemu moja (Tanzania Electronic Investment Window-TeIW) huku akibainisha kuwa utawaweka kando watu waliokuwa wakiwatapeli wawekezaji.

Kadhalika, kwenye tukio hilo lililofanyika juzi, Waziri Mkuu alizindua mwongozo wa kuwasajili watoa huduma za ushauri kwa wawekezaji na kampeni ya uhamasishaji uwekazaji.

Uzinduzi huo ulifanyika kwenye ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwamo Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jery Silaa na Waziri wa Habari, Sayansi na Teknolojia, Nape Nnauye

Majaliwa alisema serikali itaendelea kujenga mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji wa ndani na wa nje ya nchi.

"Ninawapongeza TIC kwa maono ya kuwa na mwongozo mzuri wa kusajili watoa huduma za ushauri kwa wawekezaji. Naamini mwongozo huu utarahisisha upatikanaji wa vibali katika taasisi zilizoko katika eneo la huduma na kuwezesha wawekezaji kufikia malengo yao ya kusajili miradi katika Kituo cha Uwekezaji," alisema

Alisema TIC ilikuwa na changamoto katika kutoa huduma kutokana na kutotumia mifumo ya teknolojia. Alisema kukosekana kwa mifumo hiyo, kulisababisha upotevu wa mapato kutokana na wawekezaji wengi kushindwa kukamilisha usajili wao kwa sababu mbalimbali ikiwamo kutapeliwa na watu wasio waaminifu.

"Serikali kwa kutambua changamoto hiyo, ilijielekeza katika kuimarisha utendaji wa TIC kupitia matumizi ya teknolojia. Lengo likiwa ni kuongeza ufanisi, kupunguza urasimu, kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kuongeza mapato ya Kituo," alisema.

Serikali, alisema imekuwa ikielekeza taasisi zake kuhusu umuhimu wa matumizi ya Teknolojia ili kuboresha huduma na kuongeza ufanisi hasa katika kutoa huduma za kielektroniki na kutaondoa kero nyingi zinazowakabili wawekezaji.

Prof. Mkumbo alisema TeIW itaboresha utoaji wa huduma kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi ambao wameamua kuwekeza nchini na kuondoa urasimu na ucheleweshwaji wa huduma kwa wawekezaji.

Alisema mfumo huo utasaidia wawekezaji kufikia malengo yao katika usajili wa miradi yao na upatikanaji wa vibali na leseni mbalimbali kutoka kwenye taasisi zilizo chini ya kituo cha huduma za mahala pamoja.


Mwenyekiti wa Bodi ya TIC, Dk. Binilith Mahenge, aliishukuru Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kufanya kazi hiyo ya mfumo bega kwa bega na TIC kwa kuwapatia ushauri wa kitaalamu kwa kuzingatia sheria na kanuni ya serikali mtandao.

Alisema kupitia nyenzo hizo tatu TIC inatarajia manufaa makubwa katika kuboresha utendaji kazi na hivyo kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma zake kwa wawekezaji.

Dk. Mahenge alisema kupitia mfumo wa TeIW serikali itaboresha mazingira ya uwekezaji, kwa wawekezaji kupata huduma za mahala pamoja na hivyo kuondoa vikwazo na usumbuafu uliokuwapo.

## KABWELA

Na Fadhil Mohammed



# Mabalozi wapya waahidi kuvutia uwekezaji nchini

**Na Joseph Mwendapole**

MABALOZI 10 walioteuliwa hivi karibuni kuiwakilisha Tanzania kwenye mataifa mbalimbali, wameahidi kufanya kazi kwa bidii kuvutia uwekezaji zaidi kutoka kwenye nchi hizo.

Mabalozi hao jana walipewa mafunzo na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kuhusu fursa za uwekezaji zilizopo nchini ili waende kuzitangaza kwenye mataifa wanayowakilisha.

Akizungumza kwa niaba ya mabalozi wenzake baada ya mafunzo hayo juzi, Balozi mteule wa China, Khamis Omar, alisema TIC imewapa taaarifa za fursa ambazo watazitumia kuvutia uwekezaji.

Alisema mafunzo wanayopewa mabalozi na TIC ni maelekezo mahsusi ya Rais Samia Suluhu Hassan kwamba kabla ya kwenda kwenye vituo vyao vya kazi, wajue fursa za uwekezaji na taratibu ambazo wawekezaji wanatakiwa kufuata.

"Kwa siku 10 tumekuwa kwenye mafunzo mbalimbali hasa ya diplomasia ya uchumi na leo (jana) tumekuja hapa TIC wametupa nyenzo za kutumia tutakapofika kwenye vituo vyetu vya kazi na tumhakikishie mheshimiwa Rais kwamba tutavutia uwekezaji," alisema

Balozi hiyo alisema kuna fursa kubwa ya masoko China kwa bidhaa mbalimbali zilizoongezewa thamani yakiwamo madini na sekta ya utalii ambayo imekuwa ikiingizia serikali mapato makubwa.

Alisema uhusiano baina ya China na Tanzania umekuwa wa manufaa makubwa kwa kuwa China imekuwa ikiingiza nchini bidhaa za mabilioni ya fedha na Watanzania nao wamekuwa wakilitumia soko la nchi hiyo kupeleka bidhaa mbalimbali.

"China ni nchi ya pili kwa uchumi mkubwa duniani ina fursa nyingi sana za kiuchumi kwa hiyo Watanzania tunapaswa kuendelea kuchangamkia fursa zinazopatikana nchini China tusibaki kuwa watazamani," alisema.

Habibu Mohamed anayekwenda kuiwakilisha Tanzania nchini Qatar, alisema TIC imewafumbua macho kuhusu fursa mbalimbali ambazo watakwenda kuzitangaza kwenye nchi wanazokwenda kuiwakilisha Tanzania.

Alisema mafunzo hayo yamekuwa na tija kubwa kwa mabalozi kwani wamefahamu kwa undani mageuzi makubwa yaliyofanyika kwenye sekta ya uwekezaji ikiwamo sheria mpya ya uwekezaji.

Mabadiliko hayo ya sheria ya uwekezaji, alisema yameondoa urasimu mwingi hivyo kuwa rahisi kwa wawekezaji kutoka nje ya nchi kuvutiwa na mazingira ya uwekezaji kuja kuwekeza hapa nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Gilead Teri, alisema wamewaambia mabalozi hao kuhusu maboresho yaliyofanyika na kurahisisha mazingira ya uwekezaji.

Alisema TIC inajukumu la kuhamasisha uwekezaji wa ndani na wa nje na wametoa kipaumbele kwenye sekta ya kilimo uvuvi na bidhaa za ufugaji zilioongezewa thamani.

"Pia tunahamasisha sana uwekezaji wa ndani kwenye bidhaa tunazoagiza kutoka nje kama mbolea, dawa mafuta ya kula kwa sababu kwa kufanya hivyo tunapunguza utegemezi wa kuagiza kutoka nje ya nchi," alisema.

Teri alisema sehemu ambayo wamefanikiwa zaidi katika kuhamasisha uwekezaji wa ndani ni ujenzi wa viwanda vya sukari ambapo kufikia mwakani serikali haitakuwa tena na haja ya kuagiza bidhaa hiyo nje ya nchi kwani itakuwa inajitosheleza kwa asilimia 100.

"Pia tunalenga kuhamasisha uwekezaji ambao utaongeza kiwango cha ajira nchini lakini uwekezaji utakaotuletea teknolojia mpya na tutaendelea kuwapa ushirikiano mzuri mabalozi hawa ili wavutie uwekezaji kwenye maeneo haya," alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Mafia, Zephania Sumaye (wa pili kushoto), akipokea sehemu ya msaada wa vifaa tiba kutoka kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Benki ya NMB, Benedicto Baragomwa (wa tatu kushoto), wakati wa kukabidhi vifaa tiba kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya hiyo jana na zahanati tano pamoja na madawati 100 kwa Shule ya Sekondari Kilamahewa, vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 40. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Agizo la Waziri Mkuu latekelezwa Kagera

**Na Jenesta Jasson,** MISSENYI.

AGIZO lililotolewa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akiwa ziarani wilayani Missenyi kuhusu kufunguliwa kwa kituo cha Afya cha Kakunyu na kupeleka vifaa tiba, dawa na wahudumu wa afya limetekelezwa ndani ya siku nne.

Katika maagizo yake wilayani hapa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alitoa siku tano kuhakikisha kituo hicho kinaanza kazi na kuhudumia wananchi ili kuondoa adha ya kutembea na kusafiri umbali mrefu kufuata huduma.

Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Daniel Chochole, alisema jana kuwa kituo hicho kimeanza kazi siku ya nne baada ya agizo hilo na tayari kimepokea vifaa mbalimbali na dawa hatimaye kuanza kutoa huduma.

Alisema kituo hicho kitafanya kazi saa 24 kuhudumia wagonjwa kwa kuwa wafanyakazi wamepewa nyumba ya kuishi iliyoko katika eneo hilo.

Baadhi ya wananchi kutoka eneo hilo waliishukuru serikali kwa kuwasogezea huduma za afya karibu kwa kuwa walikuwa wakipata shida kutokana na huduma hizo kutolewa mbali hali iliyokuwa ikisababisha vifo kwa wama na watoto.

"Tunashukuru kwa ujio wa Waziri Mkuu maana tatizo hili tulikuwa nalo kwa muda mrefu lakini sasa tutapata huduma karibu yetu," alisema Spryian John. Mganga Mfawidhi wa kituo hicho, Dk. Asagile Chaula, alisema wameanza kupokea wagonjwa na kuwapa huduma lakini pia aliwatoa hofu na kuwaahidi wakazi wa maeneo hayo kuwa watakuwa bega kwa bega kutoa huduma kulingana na kilicho ndani ya uwezo wao na kuhakikisha wananchi wanakuwa salama.

## Bil. 34.8/- zalipa fidia ujenzi bomba mafuta

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SHILINGI bilioni 34.8 zimetumika kuwalipa fidia wananchi 9,813 kupisha ujenzi wa bomba la kusafisha mafuta ghafi (EACOP).

Watu hao waliolipwa ni sawa na asilimia 99 ya wananchi wanaopitiwa na mradi huo huku wakisalia 83 pekee.

Mratibu wa Mradi huo, Asiadi Mrutu, alibainisha hayo juzi wakati akielezea maendeleo ya ujenzi wa mradi huo, kwenye semina na waandishi wa habari mkoani Shinyanga ya kupata uelewa juu ya utekelezaji wa ujenzi huo, iliyoandaliwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC).

Alisema mradi huo hadi sasa utekelezaji wake umefika asilimia 25 huku wakilipa fidia wananchi kwa asilimia 99 na waliosalia ni ambao bado wana migogoro ya kifamilia ikiwamo ya mirathi ya mashamba na ardhi. Alisema watu hao watalipwa fedha zao baada ya kuafikiana ndani ya familia.

"Mradi huu wa ujenzi wa bomba la mafuta haujasimama na mpaka sasa tumekamilisha mambo mengi ikiwamo ujenzi wa matangi ya kuhifadhi mafuta, kambi na karakana za mabomba," alisema Mrutu.

Pia alisema, baada ya maandalizi yote hayo kukamilika, kwa sasa wako kwenye maandalizi ya kuanza rasmi ujenzi wa bomba kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani mkoani Tanga, Tanzania likiwa na urefu wa kilomita 1,443.

Mrutu alisema bomba hilo kwa upande wa Uganda litajengwa urefu wa kilomita 296 na Tanzania kilomita 1,147. Bomba hilo linatarajiwa kuwa na uwezo wa kupitisha mapipa ya mafuta 216,000 kwa siku. Utekelezaji wa mradi huo ni miezi 24 kuanzia Januari, mwakani kwa gharama za dola za Marekani bilioni 5.008.

Alifafanua kuwa ujenzi wa bomba hilo litakuwa na awamu tatu, awamu ya kwanza kutoka Hoima hadi Mtukula kilomita 296, ya pili Mtukula hadi Singida kilomita 614 na ya tatu ni Singida hadi Chongoleani kilomita 533.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kutoka TPDC, Marie Msellemu, aliwataka waandishi wa habari mkoani Shinyanga, kuelimisha jamii juu ya maendeleo ya ujenzi wa bomba hilo, na kuondoa upotoshaji kwamba mradi umesimama.

Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari mkoani Shinyanga, Greyson Kakuru, akizungumza kwa niaba ya waandishi wa habari mkoani hapa, alisema mafunzo hayo yamewapatia ufanisi mkubwa katika utendaji kazi wa kuhabarisha umma habari sahihi juu ya utekelezaji wa mradi huo wa bomba la mafuta.



## Bil. 1/- kutumika kufunga taa, kamera za usalama Arusha

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

SERIKALI imesema inakusudia kuliongezea hadhi zaidi Jiji la Arusha, kwa kulifunga taa katika barabara zote na kufunga kamera za usalama ili kulitambulisha kimataifa kama Jiji la kitalii.

Jana, Mkuu wa wilaya hiyo, Filician Mtehengerwa, alitangaza kuwapo kwa mpango huo, akiwa katika katika Kata ya Daraja Mbili.

Alisema Jiji la Arusha linaitwa Geneva ya Afrika, ni vyema sifa hiyo ikaenda na uhalisia.

Alisema kutokana na uhitaji huo, serikali imetenga zaidi ya Sh. bilioni moja kwa ajili ya kufunga taa katika barabara zote za Jiji hilo.

Aidha, aliwataka madiwani wa Halmashauri ya Jiji la Arusha kuhakikisha wanapata mwekezaji mwenye vyombo vya kisasa vya kuzoa taka na kuchakata na siyo mwekezaji wa kuzoa taka na kwenda kutupa katika dampo, kwamba stahili hiyo imepitwa na wakati kwa hadhi ya Jiji la Arusha.

Alisema haiwezekani Jiji la Arusha kila kona majalala ya taka jambo ambalo siyo sawa, kwamba mwekezaji mwenye vyombo vya kisasa anapaswa kupewa kazi hiyo na ifike wakati madiwani wawajibike katika kumsaka mwekezaji huyo. Alisema jukumu hilo sasa liko mikononi mwa madiwani kushirikiana katika kumsaka mwekezaji mwenye sifa ikiwemo uwezo wa kuchakata taka na kuzifanya kuwa mbolea kwa wakulima.

Akizungumzia kuhusu ulinzi alisema kata inayoongoza kwa uhalifu katika Jiji la Arusha ni Kata ya Daraja Mbili, hivyo amewataka wazazi kuwaonya watoto wao vinginevyo wasimfuate kwa lolote litakalowatokea.

Amesema daraja mbili hususani Mtaa wa Ally Nyanya umekithiri matukio makubwa ambayo yamesababisha wananchi kulala mapema kutokana na kupigwa mapanga kuibiwa vifaa vya gharama na muda mwingine kuchomwa vizu.

Mtehengerwa alitoa mwezi mmoja kuhakikisha zinapigwa kura ya kuwataja wahalifu wote wa kata hiyo, kuchukuliwa hatua.

Diwani wa Kata hiyo, Prosper Msofe, alimwomba Mkuu wa Wilaya, kutoa ushirikiano na baadhi ya viongozi wa kata hiyo akiwemo Mtendaji wa Kata, John Joseph kuthibiti wahalifu kwani kata hiyo ina vijana wenye sifa mbaya ya uhalifu.

# Asilimia 40 wanaougua kifafa hawajawahi kutumia dawa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MTAFITI Mwandamizi kutoka Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu nchini (NIMR), Dk. Bruno Mmbando, amesema asilimia 40 ya watu wanaougua ugonjwa wa kifafa hawajawai kutumia dawa za kufubaza makali ya ugonjwa huo.

Amesema kutotumia dawa hizo ndio chanzo cha baadhi ya watu kuanguka maeneo mbalimbali, ikiwemo kwenye maji, moto na hata wakati mwingine kupoteza maisha.

Aliyasema hayo jana katika kikao kazi maalumu cha tathimini ya ugonjwa huo, kilichofanyika Moshi, mkoani Kilimanjaro

"Utafiti unaonyesha ugonjwa huu wa kifafa upo kwa kiwango kikubwa maeneo ambayo kuna ugonjwa wa usubi, bado kuna tatizo kubwa la uelewa kuhusu ugonjwa huu, jambo ambalo linasababisha watu kubaguliwa na kukosa fursa nyingine ikiwemo za upatikanaji wa elimu," alisema.

Akizungumzia zaidi ugonjwa huo, Mwenyekiti wa Chama cha Madaktari na Wauguzi wa Kifafa (TEA), Prof. William Matuja, alisema bado magonjwa ya mfumo wa fahamu, hasa kifafa hapa nchini ni tatizo.

Alisema kila watu 1,000, watu 20 waugua na kucheleweshwa matibabu au kukosa matibabu kutokana na ugonjwa huo kuhusishwa na imani za kishirikina.

Mwakilishi wa Wizara ya Afya, Dk. Damas Andrew, ambaye pia ni Daktari Bingwa wa Afya ya Akili na Mifumo ya Fahamu, aliishauri jamii kuachana na fikra potofu juu ya ugonjwa huo akisema unatibika na dawa zinapatikana katika vituo vyote vya afya nchini.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wananchi wa Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro akiwemo, Anastasia Lyimo, alisema kuwa bado hakuna elimu ya kutosha juu ya ugonjwa huo.



Mkuu wa Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro, Kasilda Mgeni (mbele), akiwaongoza wajumbe wa kamati ya ulinzi na usalama wa wilaya hiyo, wakati wa operesheni maalum ya kushtukiza kufuatilia taarifa za kuwepo kwa shughuli za uchimbaji madini ya dhahabu kinyume na sheria katika kata za Kisiwani na Msindo, juzi. **PICHA: ASHRACK MIRAJI**

## DC Same atahadharisha uchimbaji madini chanzo cha maji

**Na Ashrack Miraji,** SAME

MKUU wa Wilaya ya Same, Kasilda Mgeni ametahadharisha tabia ya uchimbaji madini katika eneo ambalo ni karibu na chanzo cha maji kinachotegemewa na zaidi ya wakazi 21,000 wa kata za Kisiwani na Msindo wilayani hapa.

Alitoa onyo hilo akiwa na Kamati ya Usalama Wilaya ya Same wakati wa operesheni maalumu ya kushtukiza, kufuatilia taarifa za kuwepo kwa shughuli za uchimbaji madini ya dhahabu unaofanyika kinyume na sheria.

Alisema wachimbaji hao pia wanatumia vyanzo vya maji ambavyo vipo karibu na machimbo hayo kusafishia madini wakitumia pia mercury na kuhatarisha usalama wa watumiaji wengine wa maji hayo.

"Kuingia huku kinyemela na kuharibu miundombinu ya maji ni hujuma hatutavumilia vitendo kama hivi, niwatake Jeshi la Polisi kuweka kambi kwenye eneo hili kuimarisha ulinzi kuhakikisha shughuli za uchimbaji zinakoma na waliohusika kuihujumu Serikali lazima watafutwe popote na wachukuliwe hatua," alisema.

Kadhalika, aliwaagiza wataalam wa maji kutoka wilayani kupima maji hayo haraka kubaini endapo yanafaa kwa matumizi ya kawaida kwa binadamu na kama yakionekana yana dosari yoyote basi wananchi wasiyatumie na kuangalia mbadala wa chanzo kingine.

Aidha, aliagiza wachimbaji wadogo ambao wanamiliki maeneo hayo ya uchimbaji kuhakikisha wanatimiza taratibu zote za kisheria za uchimbaji madini na kuwasilisha ofisini kwake.

Mkurugezi wa Kampuni ya Same Gold Mining Elimino, John Bina alisema: "Nakuahidi Mkuu wa Wilaya kuwa nitatoa ajira ya kutosha kwa vijana na kufanya shughuli za maendeleo katika Kata ya Msindo Kijiji cha Duma na kuwa mlinzi wa maeneo hayo".

# Kata 6 zapitisha sheria kupinga ukeketaji, ukatili kijinsia

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

MOTO wa viongozi wa mila wa jamii ya kimasai kukubali mabadiliko na kutaka kufutwa mitizamo hasi ili kuzipuuza baadhi ya mila kandamizi dhidi ya wanawake na watoto, ikiwamo ukeketaji, umeambukiza kata sita zinazokaliwa na idadi kubwa ya wafugaji katika ukanda wa tambarare wa Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro.

Jana, Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii, wilayani hapa, Marko Masue, alisema kata zinazofikiria kuunga mkono uamuzi wa kupitisha sheria ndogo kudhibiti ukeketaji na ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto ni Gararagua, Okrolili, Ormelili, Karansi, Donyomoruwa na Biriri.

"Tunafikiria nia njema waliyonayo hawa viongozi wa mila ikitimia, suala la ukeketaji litakuwa historia. Kuna vijiji vinne tayari vinavyojaliwa na jamii ya kimasai vimeshapitisha sheria hiyo,"alisema Masue

Hivi karibuni, wananchi wa Kijiji cha Loiwang' walipitisha sheria ndogo inayong'ata zaidi familia za kifugaji zinazopokea 'sukari' kwa ajili ya kuozesha watoto wenye umri mdogo, kupinga masuala ya ukeketaji na ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto.

Sheria hiyo imeweka adhabu ya Sh.100,000 ama kifungo cha miezi mitatu au vyote kwa pamoja kwa atakayepokea sukari ili mwanaye aolewe.

Akizungumzia sheria hiyo, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Loiwang' kilichoko Kata ya Donyomoruwa, Joseph Kivuyo, alisema wamefikia uamuzi huo kutokana na Kijiji hicho kutishiwa na ukatili wa kijinsia hasa kwa wanawake na watoto.

Aidha, Katibu wa viongozi wa mila (Malaigwanani) wa jamii ya Kimasai, Kata ya Donyomoruwa, Luka Mollel, alisema wameamua kuielimisha jamii yao kuachana na vitendo hivyo ambavyo ni kinyume na haki za binadamu.

"Malaigwanani tumekubaliana kwamba vijiji vyetu vije na sheria hii kwa sababu tumeona umuhimu wa elimu. Sasa tunataka waachane na mila za kuozesha watoto na wawapeleke shule," alisema. Mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha, Alfred Joshua, alisema vijiji vinne ambavyo vinakaliwa na idadi kubwa ya wafugaji wa Kimasai vilivyopitisha sheria ndogo, ni Embukoi, Donyomoruwa, Munge na Loiwang'.

Ofisa Mradi wa Haki za Binadamu Pamoja na Jinsia kutoka Shirika la KWIECO, Elizabeth Mushi, alisema wanafanya kazi ya kuzijengea uwezo jamii za kifugaji wilayani hapa, kupinga vitendo hivyo kupitia mradi wa jamii salama.

Kwa mujibu wa Elizabeth, lengo la mradi huo ni kuwaokoa wanawake na watoto wanaokabiliwa na ukatili wa kijinsia, kwa mwaka huu, tayari wamefanikiwa kuwapa mafunzo malaigwanani 48, mangariba na baadhi ya watu katika vijiji hivyo, wakiwamo wanawake wa Kimasai.



# Mil.337/- za mikopo hazijarejeshwa H/shauri Msalala

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

UREJESHWAJI wa mikopo ya asilimia kumi katika Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama imeendelea kusuasua, kati ya Sh. milioni 409 zinazohitajika kurejeshwa ni Sh.milioni 72 pekee zimerejeshwa.

Ukomo wa kurejesha mikopo hiyo unatarajiwa kuwa Novemba mwaka huu, lakini urejeshwaji wake umeendelea kuwa hafifu hali iliyofanya Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Hamis Katimba kuwakumbusha madiwani kusimamia shughuli hiyo.

**"Baadhi ya vikundi tumevipatia trekta ya kilimo na pikipiki hii itasaidia kuongeza uzalishaji katika mazao ya chakula na biashara na vijana...**

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari na kueleza kuwa katika mwaka wa fedha 2022/23 zilitengwa Sh.milioni 461 lakini mikopo iliyotolewa ni Sh.milioni 409, huku zilizorejeshwa ni Sh.milioni 72 pekee kwa kipindi hicho.

Katimba aliwataka madiwani kuhakikisha wanavisimamia vikundi vyote vilivyopewa mikopo vinarejesha kwa wakati na kuvipatia vikundi vingine fursa ya kukopa ili kujikwamua kiuchumi.

Alisema wakati wa mchakato wa kuhakikisha vikundi hivyo vinapata mikopo, madiwani walikuwa mstari wa mbele katika kuvisimamia na kuwataka kutumia nguvu hiyohiyo kuhimiza vikundi hivyo kurejesha fedha hizo.

Kadhalika, alisema halmashauri hiyo imekuja na utaratibu mpya wa kuviwezesha vikundi zana za kilimo zikiwemo trekta na pikipiki ili kudhibiti upotevu wa fedha za umma na kuwawezesha kufanya miradi yenye tija.

"Baadhi ya vikundi tumevipatia trekta ya kilimo na pikipiki hii itasaidia kuongeza uzalishaji katika mazao ya chakula na biashara na vijana watapata fedha za kuendeshea familia zao, utaratibu huu tutaendelea nao ili kuwainua vijana ili kuondokana na kushinda vijiweni wakicheza michezo ya kubahatisha," alisema Katimba.

Diwani wa Ikinda, Matrida Musoma alisema baada ya kupata maagizo ya kuhakikisha vikundi vyote vilivyopokea fedha za asilimia 10 zinarejesha wameanza kutekeleza agizo hilo kwa kuvitembelea na kujua vimekwamba wapi.

Alisema hadi kufikia Agosti mwaka huu Sh. milioni 72 zimerejeshwa na wanaendelea kuvihamasisha vikundi.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Mibako Mabubu alisema, utaratibu ulioanzishwa wa kuvipatia vikundi vya vijana zana za kilimo kama trekta na pikipiki ni mzuri na utasaidia kutopoteza fedha za umma na watazalisha zaidi mazao ya chakula na biashara na kurejesha mikopo kwa wakati baada ya kuuza mazao yao.



Ofisa Vipimo Mkoa wa Geita, Lusako Mwaioja (kulia), akikagua mizani kwenye soko kuu la dhahabu Mkoa wa Geita jana, ikiwa ni mwendelezo wa operesheni za kushtukiza ukaguzi wa mizani hizo. **PICHA: SAID SINDO**

## 'Usipopeleka mifugo kupata chanjo faini 300,000'

**Na Halima Ikunji,** UYUI

MKUU wa Wilaya ya Uyui mkoani Tabora, Zachalia Mwansasu amewaonya wafugaji ambao wamegoma kupeleka mifugo kwa ajili ya kupata chanjo ya mapele ya ngozi katika Kijiji cha Ibelamilundi, kwamba watakaoshindwa kutekeleza hatua hiyo watatozwa faini ya Sh.300,000.

Aliyasema hayo kwenye uzinduzi wa chanjo za mifugo ya mapele ya ngozi uliofanyika jana wilayani hapa na kusema kuwa hatamuonea haya mtu yeyote kwa kushindwa kutekeleza agizo hilo kwani atakuwa amekiuka sheria ya nchi.

Mwansasu alisema kwamba majosho 13 yamekarabatiwa na mengine manne yamejengwa na tayari wameyazindua katika maeneo ya Shitage, Upuge, Muhulidede na Mishwaki.

"Katika mwaka wa fedha 2023 serikali imetupatia fedha za kujenga majosho 13 kukarabati ya zamani na kwa mwaka huu kuna bajeti ya majosho 18, kadhalika zimetolewa fedha za ruzuku kwa ajili ya dawa za mifugo," alisema.

Meneja wa ghala wa maabara ya Vetinali Kanda ya Magharibi Tabora, Nae Dk. Kwari Bura, alisema kuwa wamezindua chanjo ya mifugo ya vipele ngozi na mpango huo ni kufuatia mpango wa kuchanja ugonjwa mmoja kila mwaka kati ya magonjwa 13.

Alisema kwamba kwa Wilaya ya Uyui walichanja mifugo kwa miaka mitatu mfululizo, huku kila ngombe mmoja akitakiwa kupata chanjo za magonjwa saba.

# WMA yafanya operesheni ukaguzi mizani ya madini

**Na Said Sindo,** GEITA

WAKALA wa Vipimo (WMA), imefanya operesheni ya kukagua mizani inayotumika kupima madini ya aina mbalimbali ili kuhakikisha hakuna mfanyabiashara anayepunjwa kwenye biashara hiyo.

Kaimu Meneja wa WMA Geita, Eva Ikula, aliyasema hayo wakati akizungumza kwenye Maonesho ya Sita ya Kimataifa ya Madini ambayo yalifanyika katika viwanja vya EPZA Bombambili Mwatulole mkoani Geita.

Alisema lengo kubwa la WMA kushiriki katika maonesho hayo ni kuwapa elimu wananchi na wadau wa sekta ya madini kuhusu matumizi sahihi ya vipimo pamoja na kuwaeleza majukumu yao.

"Kwa Geita yapo jumla ya masoko 10 ya kuuzia na kununulia dhahabu ambayo ni Geita Mjini, Katoro, Chato, Lwamgasa, Nyarugusu, Mbogwe, Bukombe, Nyang'wale, Mgusu na Nyakagwe na biashara hii muhimu haiwezi kufanyika bila minzani ya uhakika," alisema.

Alisema jukumu kuu la WMA katika sekta hiyo ni kuhakikisha mizani yote inayotumika kuuzia na kununulia vito na madini inahakikiwa na inapimwa kwa usahihi.

Meneja huyo alisema baada ya ukaguzi wa mizani hiyo kukamilika imekuwa ikiwekewa alama maalumu ambayo inaonyesha kuwa mzani husika umehakikiwa na unafaa kwa matumizi.

Alisema alama zinazowekwa katika mizani iliyohakikiwa ni stika pamoja na lakiri (seal) ambayo inakuwa na alama ya nembo ya taifa pamoja na tarakimu mbili za mwisho za mwaka husika mfano (23) ikiashiria imehakikiwa 2023.

Alisema uhakiki wa mizani utawezesha serikali kukusanya mapato kwa usahihi na wauzaji wa madini watapata fedha stahiki kulingana na thamani ya madini wanayouza.


Mmoja wa wafanyabiashara wa madini kutoka Soko Kuu la Dhahabu Geita, alisema wakala wa vipimo wanapita mara kwa mara kukagua mizani inayotumika kwenye biashara ya madini.

Alitoa wito kwa wafanyabiashara wengine kwenye soko hilo kuhakikisha mizani yao imekaguliwa na kuahidi kuwa balozi kwa wafanyabiashara wengine kuwahimiza kutumia vipimo sahihi wakati wote na kuzingatia matakwa ya sheria ya WMA.



Ukurasa 12

**Msomi zoolojia UDSM, Wilangali na maajabu usiyoyajua kuhusu popo**



Ukurasa 13

Ummy afunguka nchi inavyosonga kufikia malengo tiba ifikapo 2030



Ukurasa 14

**Jafo ataja msimamo wa Afrika katika safari ya kuelekea COP 28**

AFYA

# Dk. Mollel aorodhesha mapinduzi afya ndani ya Awamu ya Sita

- Ilianza bajeti Sh. Bilioni 900, sasa Sh. Trilioni 2.4
- Vifaa Upasuaji ubongo, mabingwa tiba, dharura
- Vituo tiba vipya 2491; mkoa mpya na hospitali

**Na Mwandishi Wetu**

KUNA swali linaloweza kuchukua sura ya kijamii, kiuchumi, afya na kisiasa likihoji; je Serikali Awamu ya Sita imefanya nini katika sekta ya Afya? Daima halina majibu mepesi hasa inapoangaliwa kisekta. Linahitaji ufafanuzi na tafsiri ya kimaumbile ya utendaji kisekta.

Ipo sura moja inayotafsiriwa kiujumla, ya kupanua wigo wa tija na huduma maalum ambazo zimekuwa zikitajwa, kama vile tiba ya moyo, kuongezwa na maboresho ya viwango na idadi ya huduma katika sekta.

Hata hivyo, kuboreka kwa ujumla kisekta katika Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, inachukua sura kuu tatu; ikianza na ukubwa wa bajeti inayowekezwa kisekta miundombinu kama majengo, pia vifaa na huduma za kitabibu, kama vile maabara.

Katika ufafanuzi wake Jumatatu wiki hii jijini Dar es Salaam, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, anatamka Jumatatu wiki kwamba katika bajeti kuna hatua kubwa imepigwa, ikiongezwa kila mwaka.

Hiyo ikaanza kushuhudiwa katika kipindi Rais Dk. Samia, katika bajeti yake ya kwanza kuingia katika nafasi hiyo, akatoa kipaumbele kikubwa katika huduma za afya kitaifa.

Wakati katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21 kulitengwa shilingi bilioni tisa (Sh. 900,088,240,000) kuhudumia sekta ya Afya katika bajeti ya kwanza Rais Dk. Samia, kuingia madarakani mwaka 2021/22, ikawa na Sh.Trilioni 2.1 za afya; ni wastani asilimia 233 ya bajeti iliyotangulia au nyongeza ya Sh. Trilioni 1.2.

Kufika katika mwaka wa fedha uliofuata, 2022/23 serikali ikaongeza Sh. bilioni 100 kufika Sh. trilioni 2.2. Katika mwaka wa fedha uliopo sasa, 2023/24 sekta Afya ikatengwa Sh. Trilioni 2.4, ziada ya Sh. bilioni 300, kulinganisha kile sekta ilipata katika mwaka wa fedha uliotangulia.

Kwa ujumla tangu Rais Dk. Samia kuingia madarakani, kuna nyongeza ya wastani asilimia 260, sawa na wastani wa Sh. Trilioni 1.5.



Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, akimjulia hali mtoto aliyefika na mzazi wake kupata matibabu katika Wodi ya watoto, Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma. **PICHA: MAKTABA**

**ZAO LAKE**

Mbali na uwekezaji wa bajeti, pia kuna misaada mbalimbali imekuwa ikielekezwa kwenye sekta ya afya. Naibu Waziri Dk. Mollel anasema anataja zao lake ni nyongeza sehemu za huduma za afya kitaifa, zitokanazo na uwekezaji huo.

"Kuanzia mwezi Julai 2022 hadi Machi 2023, vituo vya kutolea huduma za afya nchini zimeongezeka kufikia 11,040, ikilinganishwa na vituo 8549 mwaka 2021," anatamka Dk. Mollel, wiki hii alipotoa taarifa hiyo.

"Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kukamilisha Hospitali ya Rufani Kanda ya Kusini Mtwara na Hospitali hiyo Kanda ya Chato, tayari huduma zimeanza kutolewa," anafafanua, huku akitaja hatua kama hizo kufikiwa katika hospitali za rufani za mikoa nchini.

Kwa mujibu wa Dk. Mollel, hospitali hizo zinazonufaika kutokana na uwekezaji wa kiafya katika miaka hiyo zaidi ya miwili ya Dk. Samia, anagusa mikoa mipya ya Njombe, Songwe, Geita, Simyu na Katavi.

**MAPINDUZI VIFAA TIBA**

Katika uwekezaji ambao anautuja umegharimu serikali Sh. Bilioni 891.5, Dk. Mollel anafafanua kwamba, serikali imemudu kuimarisha nyenzo muhimu za huduma ya dharura, hali kadhalika majengo maalum.

Anataja hayo ni katika hospitali za mikoa, kanda na taifa, akieleza hadi kufika Machi mwaka huu, kulishajengwa vyumba vya wagonjwa mahututi (ICU) 73 katika hospitali hizo.

"Kuimarika huduma hizi kumeiwezesha hospitali kuokoa maisha ya wagonjwa ambao wanauhitaji huduma hizo kwa asilimia 20 hadi 40," anasema Dk. Mollel.

MAZINGIRA

# Msomi zoolojia UDSM, Wilangali na maajabu usiyoyajua kuhusu popo

• Mnyama au ndege? Analala mchana, miguu juu kichwa chini...

**Na Christina Mwakangale**

MTAALAMU wa Zoolojia wa Chuo Kikuu Dar es Salaam, Yusuph Wilangali, anamtaja kiumbehai popo ni mnyama, katika kundi la mamalia.

Anasema, tabia zake za kukaa kwenye miti akining'inia ni miongoni mwa sababu za mnyama huyo kuleta maswali kadhaa kwenye jamii.

Mwanasayansi huyo wa maabara kutoka Idara ya Zoolojia na Uhifadhi wa Viumbepori UDSM, anamfafanua popo anavyoishi ni kinyume na mazingira yaliyozoeleka, mchana analala na usiku yuko macho. Pia, akiwa na ufafanuzi wa anavyoishi kichwa chini na miguu juu. Fuatilia mazugumzo yake na Nipashe:

**Swali:** Popo ni mnyama au ndege?

**Jibu:** Ningependa kuzungumzia popo kiujumla, ili tupate ule uelewa. Popo ni mamalia kundi moja na wanyama wenye nywele, wenye chuchu wanaonyonyesha watoto wao kama binadamu, simba na swala, tofauti na uvumi kuwa popo ni ndege.

Popo mikono yao ina mabawa, na ni sifa kuu zinazomuweka kuwa mamalia na siyo ndege. Pia ana nywele na siyo manyoya kama ndege walivyo, pia wana chuchu na hunyonyesha watoto wao tofauti na ndege, kwani hawana chuchu na hawanyonyeshi.

Zipo zingine za kitaalamu zaidi ikiwamo taya la chini, kwa upande wa popo limeundwa na mfupa mmoja na kwa ndege ni zaidi ya mfupa mmoja unaounda taya ya chini. Pia, kuna sifa ya mshipa mkuu wa 'ateri'. Kwa popo, unakunjika upande wa kushoto wakati kwa ndege ni kulia. Zipo sifa zingine nyingi za kitaalamu ambazo popo zinamuweka upande wa mamalia na siyo ndege.

**Swali:** Kuna aina ngapi za popo au 'spishi' (jamiii) zao kwa ujumla na ambao zaidi wanapatikana jijini Dar es Salaam.

**Jibu:** Popo wana 'spishi' nyingi takribani 1,400 duniani ambayo ni asilimia 20 ya 'spishi' wote walio kwenye kundi la mamalia. Ni kundi la pili la mamalia lenye 'spishi' nyingi, ukiachana na kundi linaloongoza la panya.

Popo anayepatikana Upanga (Dar es Salaam) ni 'fyling fox'. Ni jina jumuishi kwa popo wote wakubwa, (megachiroptera), hivyo wanaweza kuitwa flying fox, fruit bats au mega bats. Jina lake kamili ni 'Straw-coloured fruit bat' na kwa jina la kisayansi ni 'Eidolon helvum'.

Ni ngumu watu kugundua wingi huo wa popo. Wao wapo 'active' wakati wa usiku wanatoka kutafuta chakula na mchana ambapo sisi (wanadamu) tuko 'active' (tumechangamka) tunazunguka.

Ni vigumu kuwaona kwenye maeneo yao ya kujificha. Kwa maana nyingine, ukiunganisha kundi la popo na panya, tunapata 'spishi' zaidi ya asilimia 60 ya 'spishi' wote wanaokuwa kwenye kundi la mamalia.

Kwa mantiki hiyo ni kwamba, makundi tu hayo mawili, la jamii ya panya na popo wanatengeneza zaidi ya asilimia 60, waliopo kwenye kundi la mamalia.

Hivyo tunaona wingi wao kundi la popo kuwa ndiyo pekee la mamalia wanaoweza kupeperuka kwa nguvu kitaalamu ni 'powered flight'.

Huwa wanakuwa na mtindo wa kuruka, lakini hawana nguvu ya kupaa wao ni kama parachuti, kwa mfano ndege anavyoruka anatumia nguvu kwenye mabawa yake ili aweze kwenda juu, lakini hawa popo hawawezi kwenda juu. Atapanda juu ya kitu na kuanza kushuka kwenda chini taratibu mfano wa parachuti.

Namna hii kwa kitaalamu tunaita 'passive flight' na tunaona kundi la popo ndiyo pekee ambalo lina uwezo wa kuruka kwa nguvu. Tunaweza kuwagawa popo katika makundi mawili, wakubwa na wadogo. Popo wakubwa kitaalamu ni 'mega bats' na 'fruit bats'. Tunaita 'fruit bats' kwa sababu wanakula matunda jamii ya mimea na tunawaita 'flyfoxes' kwa sababu sura zao zinafanana na mbwa.

Na kuna aina ya pili, yaani popo wadogo ambao mara nyingi wanakula wadudu na mazao mengine yanayotokana na jamii ya nyama kama damu. Hivyo, kwa kesi yetu kwa hawa popo waliopo Upanga (Dar es Salaam), wanaingia kwenye kundi la popo wakubwa.

**Swali:** Je tunawezaje kuwatofautisha popo wadogo na wakubwa?

**Jibu:** 'Mega bats' ni popo wakubwa kama lilivyo jina lao. Pia, ni wakubwa ukilinganisha na hawa wadogo, lakini hawa 'mega bats' wana kucha ambazo zimepinda kama ndoano. Hawa wadogo hawana hizo kucha. Huu 'ukucha' popo wakubwa huwa wanautumia kwenye kitu kile wanachokining'inia.

**Swali:** Je, popo hasa hawa wakubwa mlo wao ni nini?

**Jibu:** Kwa upande wa chakula wengi wa hawa popo wakubwa wanakula matunda, maua na vyakula vitokanavyo na mimea. Popo wadogo huwa wanakula wadudu au mazao mengine yatokanayo na damu. Kwa upande wa Afrika Mashariki tuna spishi 18 za hawa popo wakubwa.

Dar es Salaam, nimekutana nao ambao wamejaa sana pale upanga ni 'flying fox' na sidhani kama kuna spishi nyingine, maana sijawahi, kushuhudia kama kuna tafiti zinaweza kupata spishi nyingine nje na huyo.

**Swali:** Kwanini wanakaa kwenye miti kichwa chini, miguu juu tofauti na mamalia wengine? Hawapati kizunguzungu?

**Jibu:** Hapana hawapati kizunguzungu! Kwa sababu, tatizo lipo kwa wanyama wengine wakijining'iniza, ni kwamba mzunguko wa damu hautakuwa sawasawa, kwa kuwa 'gravity' (mvuto wa asili kuelekea ardhini) unavuta chini. Kama wewe (mwandishi), ukigeuka kichwa chini miguu juu, damu itashindwa kuzunguka vizuri na kusababisha kizunguzungu.

Lakini, popo wameumbwa wasipatwe na madhara yeyote hasa yahusianayo na mzunguko wa damu, hasa wakiwa wamening'inia ikiwamo, mfumo wa damu wenye ufanisi, hii ikiwa ina maana popo wana mfumo wa damu ambao una ufanisi mkubwa dhidi ya kanuni ya mvutano ya dunia (Gravitation force).

Ni kwa sababu wana moyo wenye misuli imara na yenye nguvu kuweza kusukuma damu dhidi ya gravity. Pia, mishipa yao ya damu ni imara. Bila shaka, unajua 'valvu' inavyofanya kazi, inaruhusu mwenendo wa damu upande mmoja tu na ikitaka kurudi valvu zake hujifunga, hivyo kuzuia damu kurudi nyuma kwenye mzunguko wake. Sababu kubwa za popo kuning'inia wanapokuwa 'wameroost' (wamepumzika) ni urahisi na ufanisi wakati wa kuruka au kupaa kwa ufanisi.

INAENDELEA UK.13



Mwanasayansi Wilangali, akiwa katika maandalizi ya kuchukua vinasaba vya popo (DNA Samples) kwa ajili ya uchunguzi.



Popo akiwa ameshikiliwa. **PICHA ZOTE: CHRISTINA MWAKANGALE.**

**Kwa mantiki hiyo ni kwamba, makundi tu hayo mawili, la jamii ya panya na popo wanatengeneza zaidi ya asilimia 60, waliopo kwenye kundi la mamalia.**

AFYA

KUTOKA KIKAON UN...

# Ummy afunguka nchi inavyosonga kufikia malengo ya tiba ifikapo 2030

**Na Yasmine Protace**

SAFARI inasonga. Katika kufanikisha ajenda za malengo ya afya kitaifa na kimataifa, wananchi wananufaika na huduma ya afya kwa wote, serikali ikitamka iko katika mapambano ya kufanikisha kutekeleza malengo ya huduma za afya kwa wote, ifikapo mwaka 2030.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akiwa kwenye kikao cha Huduma za Afya kwa wote kilichofanyika kwenye Mkutano Mkuu wa 78 wa Umoja wa Mataifa jijini New York, anatamka:

"Tanzania inaungana na wajumbe wengine wa kikao hiki katika kutekeleza azimio hili la kuhakikisha kila mwananchi anafikiwa na huduma bora za afya popote alipo."

Anaongeza kuwa upatikanaji huduma za afya kwa wananchi nchini umeendelea kuimarika kutoka asilimia 38 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 43 mwaka 2022, huku bajeti ya afya ikiendelea kuboreshwa maradufu kutoka dola milioni 529 mwaka 2019 hadi kufikia dola milioni 950 mwaka 2022.

Anasema, Tanzania imeendelea kutekeleza Azimio la Afya kwa Wote, walilowekа viongozi wakuu wa nchi kwenye Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa mwaka 2019, kwa kuboresha upatikanaji huduma za afya kwa wote, kuhamasisha wananchi kujiunga na skimu mbalimbali za Bima ya Afya.

"Serikali ya Tanzania inaendelea kutenga fedha kuhakikisha inafikia lengo la afya kwa wote ikiwamo kuwasilisha muswada wa bima ya afya kwa wote katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," anasema.

Pia, anaongeza, ili kufikia lengo la 'afya kwa wote' ni lazima huduma za afya ngazi ya msingi ziboreshwe, wananchi waweze kupata huduma bora za afya wakiwa karibu zaidi na maeneo yao, kuimarisha utoaji wa elimu ya afya pamoja na kuongeza nguvu za mapambano dhidi ya magonjwa na utoaji tiba.



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu. **PICHA: MTANDAO**

"Tunahimiza ushirikiano wa pamoja kati ya serikali na wadau wa sekta ya afya, kuungana pamoja katika kufikia malengo tuliyoweka ya afya kwa wote hadi ifikapo mwaka 2030, kwa kuwekeza kwenye ubunifu wa teknolojia mpya, rasilimali, mbinu bora za kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza pamoja na huduma za chanjo na dawa". anasema.

Akizungumza jinsi ya kutokomeza ugonjwa wa malaria, anafafanua kuwa inahitajika rasilimali zaidi na uwajibikaji wenye kuleta matokeo chanya kwenye mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

"Tunahitaji rasilimali zaidi kupambana na malaria, ugonjwa huo unaathiri asilimia 1.3 ya ukuaji uchumi barani Afrika. Ni lazima tuwekeze zaidi na kuwajibika kwenye mapambano dhidi ya malaria kwa kushirikiana na wadau wengine," anasema.

Anaongeza kuwa Tanzania inaendelea kujiimarisha kiuchumi kutokana na athari za maradhi UVIKO-19, hivyo ni dhahiri rasilimali zinahitajika zaidi kuweza kufikia malengo ya kupambana na malaria.

Kwa mujibu wa Waziri Ummy, mzoefu wa Wizara ya Afya, Tanzania inaendelea kuweka mkazo kwenye mapambano dhidi ya malaria, kwa kushirikiana na sekta binafsi, asasi za kiraia na jamii kwa ujumla juu ya kukabiliana na ugonjwa wa malaria.

**VITA MALARIA, TB**

Waziri Ummy anabainisha kuwa Tanzania karibuni imezindua Baraza la Kutokomeza Malaria, lenye jukumu la kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali zaidi, kuelimisha jamii dhidi ya ugonjwa huo, ili kuongeza nguvu zaidi za mapambano dhidi ya malaria.

"Tanzania, Afrika na dunia nzima inaweza kuwa salama zaidi bila ya ugonjwa wa malaria endapo kutakuwa na umoja kwenye mapambano dhidi ya ugonjwa huu" anasema.

Akizungumzia kutokomeza ugonjwa wa kifua kikuu ifikapo mwaka 2030, anasema kuwa

> **"Serikali inaendelea na mapambano dhidi ya ugonjwa huo na kuutokomeza ifikapo 2030.**

Jumuiya za kimataifa kushirikiana na serikali katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa kifua kikuu, kwa kuongeza nguvu zaidi ya mapambano dhidi ya ugonjwa huo na kuweza kuutokomeza kabla ya mwaka 2030.

"Bado hakuna rasilimali za kutosha kupambana na TB, tunaendelea kuhimiza wadau wa sekta ya Afya, kuunganisha nguvu za pamoja na kuwekeza zaidi kwenye rasilimali, tafiti, teknolojia, vifaa na vifaa tiba," anasema.

Anafafanua kuwa, Tanzania ni miongoni mwa nchi 30 zenye watu wengi wenye maambukizi ya kifua kikuu ikichangia asilimia 87 ya ugonjwa huo duniani.

"Takwimu za mwaka 2021 zinaonyesha kuwa Tanzania ilikuwa na watu 132,000 wanaogua ugonjwa wa kifua kikuu, tumeweza kupunguza maambukizi mapya ya ugonjwa huu kwa asilimia 32 na vifo vitokanavyo na ugonjwa huo kwa asilimia 55," anasema.

Waziri Ummy, anaendelea kufafanua kuwa: "Serikali inaendelea na mapambano dhidi ya ugonjwa huo na kuutokomeza ifikapo 2030."

Anaongeza kwamba, katika kuhakikisha ugonjwa unatokomea ifikapo mwaka 2030, anasema Tanzania imewekeza nguvu kubwa kwenye matibabu ya kifua kikuu na utoaji elimu ya afya, ili jamii iufahamu ugonjwa huo mapema na kupata matibabu.

Anaongeza kuwa Tanzania inatekeleza Mpango Mkakati Shirikishi wa Sekta ya Afya katika mapambano dhidi ya kifua kikuu uliozinduliwa mwezi Machi mwaka huu, utakaosaidia kuongoza katika mapambano dhidi ya kifua kikuu.

Hapo anatangaza msimamo wa Tanzania, kwamba inaungana na nchi nyinginezo chini ya Umoja wa Mataifa, kuendeleza mapambano dhidi ya ugonjwa huo na imeridhia azimio lililowekwa, kuendelea na mapambano dhidi ya kifua kikuu.

## Msomi zoolojia UDSM, Wilangali na maajabu usiyoyajua kuhusu popo

**INATOKA UK.12**

Maana wakitaka kuruka, kwa sababu wamejining'iniza, ni rahisi wanajiachia tu na tayari anakuwa anapeperuka tofauti na angekuwa kasimama kama ndege. Ili aweze kuruka, anatakiwa atumie nguvu kwanza kujitupa hewani, halafu ndio mabawa yaanze kazi yake kama ndege wafanyavyo.


'Ku-roosting' ni kitendo cha popo au hata ndege, kupumzika usiku ama mchana wakati hawafanyi harakati nyingine kama kula, kujamiiana ama kulala.

Pia, kwa popo kuruka kutokea chini ni jambo gumu sana kwake, kwa sababu miguu yake ni dhaifu kutosha kumpa nguvu ya kupaa mwanzoni yaani to take off. Pili, uhifadhi wa nishati ama nguvu.

Popo yeye ananing'inia bila kutumia nguvu yeyote, kwa sababu ile miguu yake na kucha zake zilizopinda (claws) 'inaji-lock' (inasikilia kama kufuli) kama wewe ukijifunga nanga kubwa halafu uitundike mahali.

Nanga itashika kama ndoano na wewe uta-relax bila kutumia nguvu kuning'inia. Tatu, sababu ya kuning'inia, ni usalama na wanyama wawindaji wengi wa ardhini hawawezi kumfikia popo akiwa juu, hivyo inawapa usalama zaidi dhidi ya maadui wa ardhini na sababu nyingine nyingi.

MAZINGIRA



Viongozi na wakuu wa Nchi za Afrika Wanachama wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi, walipokutana jijini Nairobi, Kenya mwanzoni mwa mwezi huu, kujadili namna ya kukabiliana na athari hizo. **PICHA: MTANDAO**

# Jafo ataja msimamo wa Afrika katika safari ya kuelekea COP 28

**Na Jenifer Gilla**

MKUTANO wa 28 wa mabadiliko ya tabianchi (COP28), unatarajiwa kufanyika nchini Dubai Novemba 30 hadi Desemba 12, mwaka huu kwa nchi wanachama kutoka maeneo mbalimbali duniani, kutarajiwa kujadili jinsi ya kuiokoa dunia na janga la mabadiliko ya tabianchi.

Viongozi wakuu, wasomi, wanaharakati, vijana, wanawake na taasisi zisizo za kiserikali wa nchi hizo, watakutana kujadili, kuwasilisha na kuchambua mikakati itakayosaidia kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi kusukuma gurudumu la maendeleo.

Kwa Afrika, mabadiliko ya tabianchi ni sababu kuu ya kutofikia malengo ya maendeleo endelevu kutokana na kuathiri sekta kuu za maendeleo kama kilimo, afya na mazingira huku uwezo wa kujikwamua na athari hizo ukiwa ni mdogo.

Licha ya nchi za Afrika kuwa wazalishaji wadogo wa hewa ya ukaa inayoharibu tabaka la Ozon, ni waathirika wakubwa wa mabadiliko ya tabianchi ikilinganishwa na nchi zilizoendelea ambao ndio waharibifu wakubwa wa mazingira duniani.

Kutokana na hali hiyo, mwanzo mwa mwezi huu, wakuu wa nchi wanachama wa mabadiliko ya tabia nchi Afrika walikutana jijini Nairobi, nchini Kenya kujadili mwelekeo wa nchi zao kutokana na janga hilo na kupanga mikakati itakayosaidia kuleta uhimilivu.

Kutoka Tanzania viongozi waliowakilisha katika mkutano huo alikuwa ni Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, ndiye mwenye dhamana ya kusimamia athari za mazingira nchini.

Waziri Jafo, anaiambia Nipashe katika mkutano huo, nchi wanachama walikubaliana na kutengeneza Azimio la Nairobi la mwaka 2023 lililosheheni ajenda na miongozo itakayozibana nchi zinazoendelea kukabiliana na athari hizo.

> **Kwa Tanzania visiwa vya Zanzibar (Unguja na Pemba) tunaona vinaathiriwa sana, maji ya bahari yanajaa hadi kwenye makazi ya watu, kwa kuwa maji hayo yana chumvi yanaathiri shughuli za kilimo.**

Jafo anasema katika azimio hilo na mambo mengine, wamekubaliana kwenda kuzibana nchi zinazoendelea kutekeleza makubaliono ya Paris ya kuzisaidia nchi zinazoendelea kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kupitia miradi ya kuhimili hasa sekta ya kilimo.

Anasema, kupitia azimio hilo, nchi za Afrika zitaenda na sauti moja COP 28 kuzihimiza nchi zinazoendelea kuangalia, namna ya kuzipatia nchi za Afrika teknolojia itakayotumika kuleta kilimo cha kisasa, kinachovumilia mabadiliko ya tabianchi kama vile umwagiliaji.

Jafo anasema, wamelipa kipaumbele suala la kilimo kwa sababu katika nchi nyingi za Afrika ikiwamo Tanzania, mabadiliko ya tabianchi yamewaathiri katika sekta hiyo kwa kiasi kikubwa na kusababisha uhaba wa chakula.

"Kwanza mvua zinakuwa hazitoshelezi ukizingatia kuwa Afrika kwa kiasi kikubwa kilimo kinategemea mvua," anasema.

Jafo anatoa mfano, Tanzania ambao wakulima wanategemea mvua za vuli na masika kwa kilimo kuwa kwa kipindi miaka mitatu, mfululizo hazikunyesha kwa mpangilio uliozoeleka na kwamba ziliponyesha, zilikuwa za kiwango kikubwa tofauti na matarajio.

Inatajwa kuwa suala lililoathiri uzalishaji wa mazao, hali iliyosukuma serikali kuja na mkakati wa teknolojia ya umwagiliaji.

"Hili kwa Tanzania tumeanza kulitekeleza kwa kiwango kikubwa. Zaidi ya shilingi bilioni 214 zimeelekezwa katika utekelezaji wa mifumo ya umwagiliaji, lengo ni kuongeza uzalishaji wa chakula," anafafanua Jafo.

Kuhusu mifugo inayokufa kwa kukosa malisho kutokana na ukame na kusababisha wafugaji kuhama na kuvamia mashamba ya wakulima, Jafo, anasema serikali inachukua hatua za haraka za kupeleka huduma za kijamii katika maeneo yao, ili kukabiliana na changamoto hiyo.

"Tumechimba malambo Wilaya ya Simanjiro (Manyara) kudhibiti wafugaji kuhama na wenzetu, Wizara ya Mifugo wametengewa zaidi ya shilingi bilioni 9.9, kwa ajili ya utengenezaji wa malambo 16 ya wafugaji na serikali imedhamiria kuwekeza miundombinu sahihi ya ufugaji," anasema.

Analitaja lingine walilolijadili katika mkutano huo, kuwa ni kuhakikisha wanaungana kama bara, ili kusaidia vijana na wanawake kuongeza ushiriki wao katika uzalishaji wa mazao ya chakula, biashara na kuzikwamua nchi zao katika umasikini .

Katika hilo Jafo, anasema Tanzania imeanza kuonyesha mfano kupitia mradi wa 'Jenga Kesho' ulio bora, kutoa fursa kwa makundi hayo, kujifunza kwa vitendo kilimo na uvuvi, kisha inawapatia mitaji na vitendea kazi vitakavyowawezesha kujitegemea kimaisha.

Anasema, pia serikali inatoa mbolea ya ruzuku kwa wakulima wote nchini, ili kuongeza uzalishaji wa mazao na kuwapa hamasa ya kuendelea na shughuli hiyo na kuwaondolea, hali ya kukata tamaa kutokana na ukame kwa kukosa mvua, mazao kuvamiwa na wadudu waharibifu na mafuriko.

Kwa mujibu wa Jafo, mkutano huo, pia walijadili watakavyowapatia wanawake fursa za kutumia nishati safi za kupikia, kupunguza matumizi ya kuni na rasilimali misitu na joto duniani.

Anasema, wanatarajia kwenda kuzibana nchi zinazoendelea, ili kuhakikisha zinatimiza ahadi yao ya kuchangia fedha za mfuko wa majanga na kupunguza makali ya Maisha, kwa watakaoathirika na mafuriko na mazao kushambuliwa na wadudu.

"Tumejipanga tutakapokwenda 'COP 28' tuhakikishe mfuko huo unazinduliwa mwaka huu kwa sababu utasaidia sana maeneo ambayo yameathirika kwa kiasi kikubwa barani Afrika.

"Kwa Tanzania visiwa vya Zanzibar (Unguja na Pemba) tunaona vinaathiriwa sana, maji ya bahari yanajaa hadi kwenye makazi ya watu, kwa kuwa maji hayo yana chumvi yanaathiri shughuli za kilimo," anasema.

Akihutubia katika Mkutano wa 78 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UN) jijini New York nchini Marekani wiki iliyopita, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, anatoa wito kwa mataifa duniani kupunguza uzalishwaji wa hewa ukaa na kuborosha uhimilivu ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Anawambia viongozi wakuu hao, waliohudhuria mkutano huo kuwa ripoti iliyotolewa hivi karibuni na Jopo la Kiserikali la Kimataifa linalofanya utafiti wa athari za mabadiliko ya tabianchi (IPCC), imebaini dunia imeshindwa kudhibiti joto lisizidi nyuzi 1.5, kama ilivyokubaliana kupitia makubaliano ya Paris.

Anasema ripoti hiyo imeonyesha mabadiliko ya tabianchi yanaendelea kuiathiri Afrika na kurudisha nyuma juhudi zake za kujiletea maendeleo, hata kushindwa kuyafikia malengo maendeleo endelevu.

### KUTOKA UN

Mshauri Maalumu wa Afrika kwa Katibu Mkuu wa UN, Naibu Katibu Mkuu, Cristina Duare, amezishauri nchi za Afrika kutotegemea misaada ya nchi zinazoendelea, kwa kuwa haitabiriki badala yake kujitafutia njia za kukabiliana na athari hizo.

Kupitia Jukwaa la Mifumo ya Chakula, anawashauri mawaziri wa fedha wa Afrika kutumia rasilimali zilizopo kutafuta fedha za kuongeza katika utekelezaji wa bajeti za wizara badala ya kusubiri mgawanyo kitaifa na kimataifa, kwa kuwa wakati mwingine fedha zinazotolewa hazitoshelezi mahitaji.

"Mawaziri wa fedha katika nchi za Afrika wanapaswa kuwa watu wa kujaribu, kama hawatakuwa wa aina hiyo basi hatutafika. Kama nina bajeti nina jukumu la kutafuta rasilimali kwenye bajeti ya taifa, siwezi kusubiria hizo fedha, wakati mwingine mgawanyo unakuwa mdogo," anasema.





## Vijana watakiwa kuchangamkia fursa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

JUMUIYA ya Vijana wa Kiislamu Wilaya ya Dodoma (JUVIKIBA) wameaswa kuchangamkia fursa zinazowazunguka kwenye maeneo yao ili kujikwamua kiuchumi.

Mwenyekiti wa jumuiya hiyo, Rashidi Ally aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na vijana waliojitokeza kufanya usafi wa mazingira eneo la makaburi ya waathirika wa ajali ya treni jijini hapa.

Usafi huo ni sehemu ya maandalizi ya kuelekea Sikukuu ya Maulidi itakayofanyika kitaifa leo jijini Dodoma na Rais Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

Akizungumza na vijana hao, alisema wanapaswa kuwa mfano kwa kufanya kazi kwa bidii ili kujikwamua kiuchumi na kuzitumia fursa zilizopo kwenye maeneo yao.

"Pia vijana wa kiislamu onesheni mfano kwa vitendo katika kuhakikisha amani iliyopo inalindwa kwa gharama yoyote na kushiriki shughuli za kijamii," alisema.

Alisema vijana wanapaswa kumuunga mkono Mufti Mkuu wa Tanzania, Shehe Dk. Abubakar Bin Zuber ambaye amekuwa akisisitiza waumini wa dini ya kiislamu kujitambua, kubadili na kuacha mazoea.

Naye, Katibu wa Jumuiya hiyo, Bashuru Mdoe aliwakumbusha vijana kuunda vikundi ili kupatiwa mikopo ambayo itakayowawezesha kuanzisha miradi itakayowakwamua kiiuchumi badala ya kukaa na kulaumu serikali kwa kushindwa kuwajali.

Alisema hivi sasa Dodoma kuna fursa mbalimbali zikiwamo za kidini na kiserikali wakiungana kwa pamoja watapata mikopo ambayo inatolewa ndani ya halmashauri na taasisi za kifedha.

## DC ahimiza wakulima kujiandikisha kupata mbolea ya ruzuku

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Wilaya ya Singida, Paskasi Muragili amewaagiza viongozi wa Halmashuri ya Manispaa ya Singida kuwaelimisha na kuwahimiza wakulima kujiandikisha kwenye daftari ili kupata mbolea ya ruzuku kwa msimu wa kilimo wa 2023/24.

Alitoa agizo hilo juzi alipokuwa akizungumza na madiwani, maofisa kilimo, watendaji wa kata na wenyeviti wa mitaa na vijiji wa kata za pembezoni mwa manispaa hiyo.

Muragili alisema suala la wananchi wanaojishughulisha na kilimo kujiandikisha kwenye daftari la wakulima ni maamuzi ya serikali na ni lazima kwa kila mkulima kujiandikisha kwa kuwa mipango yote katika sekta ya kilimo nchini itatokana na takwimu za daftari hilo.

Alisisitiza ushirikiano kati ya viongozi na wananchi ili kukamilisha kwa haraka na kwa ufanisi uandikishaji huo.

Aidha, alielekeza manispaa hiyo kuhakikisha wakulima wote watakaojiandikisha katika daftari waingizwe katika mfumo ili kuondoa kero zilizojitokeza msimu wa kilimo mwaka jana.

Muragili alisema serikali imetenga bajeti kubwa kwa ajili ya sekta ya kilimo kwa mwaka wa fedha 2023/24 kutokana na kutambua kuwa asilimia kubwa ya wananchi wanajishughulisha na kilimo na wanategemea kilimo kwa ajili ya kipato chao.

# Mavunde aanza mkakati wa kuinua bei tanzanite sokoni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Madini, Anthony Mavunde amekutana na wadau wa madini ya tanzanite ili kuweka mikakati ya kukabiliana kuporomoka kwa bei ya madini hayo.

Hatua hiyo imekuja baada ya hivi karibuni baadhi ya wachimbaji wadogo wa madini ya tanzanite kuiomba serikali kunusuru kuporomoka kwa bei ya madini hayo.

Akizungumza na Nipashe kuhusu mikakati ya kukabiliana na hali hiyo, Mavunde alisema wameanza kuwashirikisha wadau kuona namna ya kuja na minada ya madini ya vito ili kuongeza masoko.

> **"Tutaendelea kuboresha uongezaji wa thamani kwa kuwajengea uwezo Watanzania, tuna Kituo cha TGC kipo Arusha...**

"Tanzania imebarikiwa kuwa na madini ya tanzanite ambayo yanapatikana Tanzania peke yake, haya ni kati ya madini ambayo tutayasimamia kuhakikisha kwanza tunasimamia changamoto iliyopo hivi sasa ya kuporomoka kwa bei, tumekuwa tukikaa vikao na wadau ili kujua namna ambavyo tutashauriana kwa pamoja ili kuinua thamani ya madini yetu haya," alisema.

Aidha, alisema ipo mikakati mbalimbali ya kuzuia utoroshaji wa madini hayo ili nchi ipate mapato na wanayapa kipaumbele kikubwa ili yawe na tija kwa Watanzania.

"Tutaendelea kuboresha uongezaji wa thamani kwa kuwajengea uwezo Watanzania, tuna Kituo cha TGC kipo Arusha, lengo kubwa ni uongezaji wa thamani ya madini ili tusisafirishe yakiwa ghafi na kuchochea ajira za Watanzania,"alisema.

Mavunde alisema serikali itaendelea kutoa kipaumbele kwa madini ya vito kwa kuwa na maonesho makubwa ya madini ya vito ili kuyatangaza na kutambulika duniani.




Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Deogratius Ndejembi (kushoto), akikata utepe kuzindua kitabu cha kumbukumbu za sauti za walengwa wa mradi wa USAID/Lishe endelevu, jijini Dodoma juzi. Kulia ni Mkurugenzi wa mradi huo, Joyceline Kaganda. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Halmashauri yapima afya ya udongo kujiandaa na kilimo

**Na Renatha Msungu,** KONDOA

HALMASHAURI ya Mji Kondoa imeanza kuchukua sampuli za udongo kwa ajili ya kupima afya katika kata nane za wilaya hiyo kabla ya msimu ujao wa kilimo kuanza.

Mkuu wa Idara ya Kilimo na Mifugo wa Halmashauri hiyo, Monica Kimario alitoa kauli hiyo mjini hapa alipokuwa akizungumza kuhusu upimaji afya ya udongo kupitia vifaa vilivyotolewa na serikali.

Kimario alisema utaratibu wa uchukuaji wa sampuli za udongo kwa kata zote nane umeanza ambapo hadi sasa tayari wamechukua udongo katika kata tano kati ya nane zilizopo kwenye eneo hilo.

Alitaja kata hizo kuwa ni Kingale, Serya,Suruke, Kolo na Bolisa, huku akisisitiza wanaendelea kwenye kata za Kondoa ambazo zimebakia.

"Tumeanza utaratibu huu ili kuhakikisha wakulima wanafanya kilimo chenye tija msimu huu ambacho kitawainua kiuchumi,"alisema Kimario.

Alifafanua kuwa halmashauri hiyo imeanza kutoa huduma ya kupima udongo katika mashamba ya wakulima bila gharama yoyote, lengo likiwa ni kuongeza tija katika uzalishaji kwa wakulima.

Alisema vifaa vilivyotolewa na serikali vinasaidia kujua, kuonyesha eneo hilo udongo wake una mapungufu kiasi gani ili wataalamu wa kilimo wajue nini kifanyike na wakulima wazalishe kwa tija.

"Zoezi hili ni endelevu hivyo wakulima ambao tumeshapita kwenye kata zao na wanahitaji huduma hii wawaone maofisa ugani wa kata zao ili udongo ukachukuliwe kwenye mashamba yao na watapewa majibu, wale wa kata zilizosalia wajiandae kwa ajili ya utaratibu huo na linafanyika pia kwa taasisi ambazo zinajishughulisha na kilimo," alisema Kimario.

Naye, Mkulima Luvuva Sure alisema utaratibu wa upimaji afya ya udongo utamsaidia mkulima kufanya kilimo chenye tija, ambacho kitamuinua kiuchumi yeye na familia yake.

Hivyo, aliwaasa wakulima wengine kutoa ushirikiano pale wataalam wa kilimo wanapopita kwa ajili ya utaratibu wa kupima afya ya udongo katika mashamba ya wakulima.

Alisema: "Tunaishukuru sana serikali kutokana kutoa vifaa vya kupima afya ya udongo vitatusaidia sana kuondokana na kilimo cha mazoea badala yake tufanye kilimo cha kisasa".

Alisema hivi sasa wakulima wanapaswa kutumia na kufuata kanuni za kilimo ambazo hutolewa na wataalam ili kupiga hatua katika kilimo chao.





# TRA yawaonya w'biashara kupitisha bidhaa njia za panya

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

WAFANYABIASHARA wanaoingiza bidhaa mbalimbali kutoka Malawi kupitia mpaka wa Kasumulu wilayani Kyela, wametakiwa kuepuka kupitisha bidhaa zao kwenye njia za panya ili wasikumbwe na mkono wa sheria.

Aidha, wametakiwa kuhakikisha wanatoa risiti za kielektroniki (EFD) wanapouza bidhaa zao ili kuisaidia serikali kukusanya mapato ambayo yatasaidia kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Meneja wa Mamlaka ya Mapato nchini (TRA) wa Wilaya ya Kyela, Novert Albert aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kuhamasisha wananchi kutii sheria za kodi ijulikanayo kwa jina la 'Tuwajibike' wilayani humo.

Alisema baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wakiingiza bidhaa kutoka Malawi kupitia kwenye vipenyo ambavyo siyo rasmi hali ambayo inaisababishia serikali hasara kwa kukosa mapato.

Alisema bidhaa hizo zinapoingizwa nchini bila kulipiwa kodi zinaharibu ushindani wa kibiashara na bidhaa ambazo zinaingizwa kihalali na hivyo kuharibu uchumi wa nchi.

**"Kumbukumbu hizo zinawasaidia wafanyabiashara kufanyiwa makadirio ya kodi ambayo ni sahihi, kwahiyo wafanyabiashara wanatakiwa wazingatie utaratibu huu," alisema Nshangaki.**

"Kwa sasa tunahamasisha wafanyabiashara kutoa risiti wakati wa kuuza bidhaa zao na wanunuzi kudai risiti, lakini nitumie nafasi hii kuwahamasisha wafanyabiashara wanaoingiza bidhaa kutoka Malawi wasitumie vipenyo visivyokuwa rasmi," alisema Novert.

Alisema wafanyabiashara hao ambao wanapitisha bidhaa kwenye vipenyo hivyo wakikamatwa ni lazima wachukuliwe hatua mbalimbali za kisheria ikiwemo kupelekwa mahakamani na bidhaa zao kutaifishwa.

Akizindua kampeni hiyo, Meneja Msaidizi wa TRA, idara ya huduma kwa walipa kodi Mkoa wa Mbeya, Princepius Nshangaki alisema wafanyabiashara wanapotoa risiti wanaisaidia serikali kukusanya mapato.

Alisema risiti hizo pia zinawasaidia wafanyabiashara wenyewe kuweka vizuri kumbukumbu za mauzo yao ya mwaka kutokana na mashine hizo kuwa na vitunza kumbukumbu tofauti na ilivyokuwa wakati wa matumizi ya risiti za karatasi.

"Kumbukumbu hizo zinawasaidia wafanyabiashara kufanyiwa makadirio ya kodi ambayo ni sahihi, kwahiyo wafanyabiashara wanatakiwa wazingatie utaratibu huu," alisema Nshangaki.

Alisema risiti za makaratasi zilizokuwa zinatumika zamani zilikuwa zinaweza kupotea ama kitabu kikajaa na hivyo mfanyabiashara akashindwa kutoa risiti tofauti na za sasa ambazo ni za kisasa.

Wakizungumzia kampeni hiyo baadhi ya wafanyabiashara wa Soko Kuu la Kyela, waliwashukuru maofisa wa TRA kwa kuanzisha kampeni hiyo wakidai kuwa itawasaidia wao wenyewe pamoja na wateja wao kufanya biashara halali.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara wa Wilaya ya Kyela, Abinote Mwakilewa alisema elimu inayotolewa na maofisa hao inasaidia kuwaamsha wafanyabiashara na wanunuzi wao kuzifahamu sheria na kuzitekeleza.

Alisema serikali inategemea kukusanya kodi kupitia risiti ambazo wafanyabiashara wanazitoa na kwamba kodi hizo ndizo zinatumika kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Naye Jane William alisema mfumo wa utoaji wa risiti za kielektroniki ni rahisi kutokana na kuwa na uwezekano wa kutumiwa na watu ambao wana elimu ya kawaida.



Maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Mbeya, wakionyesha mabango ya kuhamasisha wafanyabiashara kuhusu utoaji wa risiti za kielektroniki, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya 'Tuwajibike', katika Soko Kuu la Wilaya ya Kyela, jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## H/shauri Njombe yatoa tahadhari wanaotupa taka mtaani

**Na Elizabeth John,** NJOMBE.

HALMASHAURI ya Mji Njombe mkoani Njombe imesema haitamvumilia mwananchi yeyote atakayeonekana kuchafua mazingira kwa kutupa taka ovyo mitaani na kwenye maeneo yasiyo rasmi.

Onyo hilo lilitolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe Kuruthum Sadick, wakati wa kufanya usafi eneo la bonde linalopita Mtaa wa National Housing, Kata ya Njombe Mjini.

Alisema kila mwananchi anawajibu wa kuhakikisha anafanya usafi kwenye maeneo yanayomzunguka na kutunza maeneo ya mabonde na vyanzo vya maji kwa kuacha kutupa takataka ovyo.

Alisema wananchi wanapaswa kutambua kwamba kutupa taka kwenye bonde hilo siyo sahihi kwa sababu halmashauri imetenga eneo rasmi kwa ajili ya kutupa taka, hivyo bonde hilo lisitumike kutupia taka.

Hata hivyo alifafanua kwamba ili kuhakisha Mji wa Njombe unaendelea kubaki katika hali ya usafi, halmashauri itaendelea kuhamasisha na kushiriki usafi wa pamoja kila mwezi ili kuwakumbusha wananchi kuwa wanawajibu wa kutunza mazingira na kufanya usafi mpaka kwenye maeneo yanayowazunguka.

Ofisa Afya wa Mkoa wa Njombe, Saada Milanzi, alisema ili kuendelea kutunza mazingira halmashauri zote za Mkoa wa Njombe ziendelee kutumia sheria ndogo zilizopitishwa ili kuwawajibisha na kudhibiti utupaji taka kwenye maeneo yasiyo rasmi.

# Shamba la mbegu laanzishwa kuwakomboa wakulima

**Na Mwandishi Wetu,** TANGANYIKA

MKUU wa Wilaya ya Tanganyika iliyopo mkoani Katavi, Onesmo Buswelu amesema ufunguzi wa shamba la mbegu la Luhafwe lililopo wilayani humo, litawanufaisha kwa kiasi kikubwa wakulima wa mkoa huo.

Buswelu aliyasema hayo wakati wa ziara ya uongozi wa Wakala wa Mbegu za Kilimo nchini (ASA), walipotembelea shamba hilo kwa ajili ya ufunguzi ili lianze kutumika.

Alisema uzalishaji wa mbegu utakaofanywa katika hilo chini ya usimamizi wa wakala wa mbegu nchini, kutasaidia kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa mbegu bora za mazao mbalimbali hapa nchini.

"Nawashukuru sana ASA kwa kufungua shamba hilo, sisi kama wilaya tutatoa ushirikiano kama kawaida ili kuhakikisha malengo ya ASA katika uzalishaji Mbegu yanafikiwa,"alisema Buswelu.

Alisema ASA ni taasisi muhimu katika sekta ya kilimo ambapo wakazi wa Mkoa wa Katavi na Kanda ya Magharibi watanufaika sana kwa uwepo wa shamba hilo.

Kutokana na hilo, aliitaka ASA kuanza haraka ufunguzi wa shamba hilo Ili msimu huu lianze kufanya kazi ya kuzalisha mbegu bora za kilimo.

Aidha, Onesmo alisema kuanza kwa shamba hilo kutaongeza fursa za kiuchumi na ajira kwa jamii ya Luhafwe na Tanganyika hasa Kwa vijana, wanawake na wazee katika sekta hiyo muhimu ya kilimo.

Mkuu wa wilaya hiyo amewataka wakazi wa maeneo hayo kuchangamkia fursa za uwekezaji kwenye uzalishaji mbegu zitakazotolewa na ASA

Kwa upande wake Mtendaji Mkuu wa ASA, Dk. Sophia Kashenge, alimpongeza Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika kwa ushirikiano mkubwa wakuhakikisha ASA wanapata shamba hilo kwa ajili ya kuzalisha mbegu.

Alisema ASA itaanza kufungua hekta 200 kwenye shamba hilo ili lianze kutumika kuzalisha mbegu katika msimu ujao wa Kilimo kwa ajili ya kuzitawanya kwa wakulima.

Dk. Sophia aliwahakikishia wananchi wa Wilaya ya Tanganyika kutoa ushirikiano na kuwapatia fursa zote zitakazopatikana shambani hapo kama ilivyo maeneo mengine ya mashamba ya wakala.

Pia aliwataka wakazi wa maeneo hayo kuchangamkia fursa ambazo zitatolewa na serikali kwa ajili ya uzalishaji mbegu bora za mazao mbalimbali.

Dk. Kashenge alisema ASA inaendelea na ziara kwa ajili ya kutembelea mashamba mbalimbali ili kuyafungua kwa lengo la maandalizi ya msimu ujao wa kilimo.

# Waziri awapa vijana ujanja wa kufanikiwa kimaisha

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VIJANA wametakiwa kuchangamkia fursa za uchumi wa buluu kwa kujikita katika uvuvi wa bahari kuu pamoja na kilimo cha mazao ya baharini, ambacho kitaleta mageuzi makubwa ya kiuchumi na kubadilisha maisha yao.

Ushauri huo umetolewa na Waziri wa Uvuvi na Uchumi wa Buluu, Suleiman Masoud Makame katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akiwasilisha na kujibu hoja za Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Waziri huyo alisema katika kutekeleza dhana ya uchumi wa buluu, kuleta mageuzi makubwa kwa

**Alisema fursa za wakulima wa mwani hivi sasa ni kubwa kufuatia ujenzi wa kiwanda cha kusarifu na kuchakata mazao yanayotokana na mwani kiliopo...**

wavuvi tayari boti 850 zimeshatengenezwa ikiwemo 500 zenye urefu wa mita tano za wakulima wa mwani ambacho kwa asilimia 80 kinalimwa na wanawake vijijini.

Aidha, alisema boti 282 zenye urefu wa mita saba pamoja na boti za urefu wa mita nane zipatazo 68 zimetengezwa kwa ajili ya wavuvi wanaovua katika maeneo yenye kina kirefu cha maji.

Aidha, alisema hizo ni sehemu ya juhudi ambazo lengo lake kubwa kuwawezesha wavuvi kuvua katika maji yenye kina kikubwa cha bahari na kuepuka migogoro inayotokana na wavuvi kushindwa kufika maeneo yenye idadi kubwa ya samaki.

Waziri huyo alisema wavuvi katika kuona wanapata mafanikio wamepatiwa vifaa vya uvuvi ambavyo vitaonyesha wapi wapo samaki wengi kwa ajili ya kuwavua pamoja na mitego salama rafiki kwa mazingira ya baharini.

Alivitaja vifaa ambavyo wavuvi wameanza kupatiwa ni pamoja na "Fish finder"kifaa ambacho kinao uwezo wa kuwajulisha wavuvi wapi wapo samaki wengi pamoja na mitego ambayo haina madhara na athari za uvuvi haramu zenye kuathiri mazalia ya samaki.

Hata hivyo aliwataka wakulima wa mazao ya baharini kuchangamkia fursa za kilimo cha mwani ambacho kwa asilimia 80 hulimwa na wanawake katika maeneo pembezoni mwa fukwe za bahari.

Alisema fursa za wakulima wa mwani hivi sasa ni kubwa kufuatia ujenzi wa kiwanda cha kusarifu na kuchakata mazao yanayotokana na mwani kiliopo Chamangwe Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Alisema Sh.bilioni 2.8 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi huo ambao unaendelea kwa kasi, huku kukiwa na uwezo wa kusarifu tani 30,000.

Aidha, alisema Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Buluu tayari imeingia makubaliano na Shirika la Misaada la Korea (KOICA) kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda kingine cha uzalishaji wa bidhaa za mwisho zinazotokana na mwani.

## Wakazi Pemba kufikishiwa miundombinu barabara, miradi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi imesema maeneo yote ya uwekezaji yaliopo Pemba yatafikishiwa miundombinu ya barabara kwa ajili ya kuwavutia wawekezaji, kuwekeza miradi ambayo itaimarisha uchumi.

Hayo yalisemwa katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed wakati akitoa ufafanuzi kuhusu kazi zinazofanywa za ujenzi wa miundombinu katika Kisiwa cha Pemba ikiwa ni sehemu ya juhudi za kukifunguwa kisiwa hicho kiuchumi na uwekezaji.

Alisema azma ya serikali ni kukifungua Kisiwa cha Pemba kiuchumi na uwekezaji ambapo mikakati imewekwa katika kujenga barabara kwa kiwango cha lami.

Alisema tayari barabara yenye urefu wa kilomita 45 kutoka Chake Chake hadi Wete imeanza kujengwa kwa kiwango cha lami ambayo inakwenda kuunganisha mikoa miwili ya Pemba katika mawasiliano ya barabara.

Hivyo, alitoa mfano wa barabara katika Kisiwa kidogo cha Kuji Pemba ambayo imeanza kujengwa, tayari baadhi ya wawekezaji wameanza kuwekeza miradi ya ujenzi wa hoteli zenye hadhi tofauti.

Aidha Dk. Mohamed alisema ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 7.5 inayokwenda katika maeneo huru ya kiuchumi na uwekezajni Micheweni ipo katika hatua za mwisho kukamilika ambayo itafungua uwekezaji katika maeneo hayo.

Alisema Micheweni ni maeneo huru ya uchumi ambapo yametengwa kwa ajili ya wawekezaji kuwekeza katika miradi mbalimbali yenye tija itakayokuza pato la taifa.



Waziri wa Ardhi na Makazi Zanzibar, Rahma Kassim Ali akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yawaomba waandishi kusaidia kutoa elimu ya ardhi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Rahma Kassim Ali amewataka waandishi wa habari kusaidia kutoa elimu kwa jamii ili kufuata sheria za ardhi zilizowekwa ili kujiepusha na migogoro isiyo ya lazima.

Akifungua mafunzo kwa waandishi wa habari kuhusu masuala ya ardhi, alisema kuna changamoto nyingi za migogoro ya ardhi katika jamii kunakotokana na jamii kukosa uelewa juu ya masuala ya sheria ikiwemo uvamizi katika maeneo ya misitu na kilimo.

"Maeneo mengi yanavamiwa kwa kasi mno hapa Zanzibar na tayari serikali imeanza ukaguzi ili kuona heka zilizobaki zinadhibitiwa ili zisiweze kupotea," alisema.

Waziri Rahma alisema wapo watu wajanja wanaotumia fursa ya kuilaghai jamii kwa kuuza maeneo ya ardhi ambayo kisheria hayaruhusiwi kuuzwa ikiwemo maeneo ya uwekezaji.

Alisema waandishi wa habari ndio sauti ya jamii ni muhimu kupewa elimu ambayo itasaidia kuwawezesha wananchi kufahamu kupitia vyombo vyao.

Aidha, alisema waandishi wa habari ni sehemu ya jamii na pia ni watu wenye mchango mkubwa, hivyo wanapokuwa na uelewa wa masula ya ardhi watakuwa msaada mkubwa kwa kuelimisha.

Hivyo, aliwataka waandishi wa hahari kuacha kutoa taarifa ambazo sio sahihi zinazohusiana na ardhi zitakazoweza kuleta migogoro baina ya serikali na wanachi, badala yake kufika sehemu husika ili kupatiwa elimu.

Alisema serikali kupitia wizara yake ipo katika mpango wa kuyapima maeneo yote ya Unguja na Pemba kwa lengo la kudhibiti maeneo yasiendee kuvamiwa.

Naye Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Ardhi Zanzibar, Khamis Juma Khamis, alisema lengo la mafunzo hayo ni kutoa taaluma kwa vyombo vya habari ili kushirikiana pamoja katika kuelimisha jamii juu ya shughuli zinazofanywa na kamisheni hiyo.

Alisema, kamisheni hiyo ni chombo kinachofanya kazi kwa mujibu wa Sheria Namba 6 ya Mwaka 2015 yenye lengo kuu la kuweka usimamizi wa ardhi katika chombo kimoja.


Alisema, kabla ya kuanzisha kwa sheria hiyo usimamizi wa utendaji wa sekta hiyo ulikuwa katika mfumo wa kiidara ambao utendaji wake ulionekana haukiwa na ufanisi mzuri. Aidha, alisema ardhi ya Zanzibar imekuwa ni moja kati ya rasilimali muhimu na mhimili mkuu wa taifa ambao umewekewa usimamizi imara ili kuilinda kwa maslahi ya wananchi na taifa kwa ujumla.

Alisema wizara kupitia Kamisheni ya Ardhi inatarajia kuzindua kampeni ya uhaulishaji wa ardhi Oktoba mwaka huu katika maeneo yote ya Unguja na Pemba na kuanza katika Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja.

Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Mzee Ali Haji, alisema anaamini waandishi wa habari watakuwa mabalozi wazuri kuona sheria za ardhi zinafuatwa kikamilifu na waandishi wa habari ni chachu ya mafanikio kwa sekta yoyote nchini.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**JAPHET PETER LIHANJALA** anatangaza kupotea kwa cheti cha **BACHELOR DEGREE** chenye usajili namba 2015178180 kilichotolewa na **SHANGHAI LIXIN UNIVERSITY OF ACCOUNTING AND FINANCE** mwaka 2019 na cheti cha MASTERS DEGREE chenye usajili namba **1901213957** kilichotolewa na PEKING UNIVERSITY mwaka 2022. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **KMR/RB/7520/237**

## KUPOTEA KWA VYETI



**JAPHET PETER LIHANJALA** anatangaza kupotea kwa vyeti vya kidato cha nne chenye index namba **S0342-0127** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **SHAABAN ROBERT SECONDARY SCHOOL** mwaka 2012 na kidato cha sita chenye index namba **S0342-0534** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia SHAABAN ROBERT SECONDARY SCHOOL mwaka 2015. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **KMR/RB/7520/237**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KIBO SEED COMPANY LIMITED** INATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 103 DQF FORD** RANGER 2.2L PICK-UP. KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KWA RB NAMBA **MAN/BAB/RB/253103/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **MRISHO KIDAU MOHAMEDI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **HUONIAO** yenye namba ya usajili MC 109 CSV.
Engine Na. **G7EPCJL06LA009876**
Chassis Na.***G7157FM1LXA800168.*** Kwa yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa kitu cha Polisi kilicho karibu.
Taarifa Polisi: LOSS REPORT:

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HANCE JOSEPH DANIEL anatangaza kupotea kwa** kadi ya pikipiki yenye jina la umiliki UWAPA SACCOS LIMITED namba yake ya usajili ni **MC 691 CKY,** CHASSIS NAMBA: **MD2A21BY3KWG90993** na ENGINE NAMBA: **PFZWKG40514.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **PHQ/ARU/ARU/3050/2023**.

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**LILILOKO DODOMA**

**MAOMBI MADOGO NA. 276 YA 2023**

**JOHN B. MILINGA ............................................MDAI**

**DHIDI YA**

**JUMA MGUNDA ........................................MDAIWA 1**
**TUSIBWENE BROWN MWAKIPESILE.......... MDAIWA 2**

**KWA: JUMA MGUNDA**

**TUSIBWENE BROWN MWAKIPESILE**
**POPOTE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**Kwa kuwa** muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 04.10. 2023 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANGALIZO:** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 22 ya mwezi wa September, 2023.

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA, LA IRINGA**
**LILILOKO IRINGA**

**MAOMBI NA:43/2023**

**ALEXANDER KAFUPI GAUDENCE..............................MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**1.MUCOBA BANK PLC...........................................MJIBU MAOMBI**
**2.SPYTECH SECURITY SUPPLIES LTD.................MJIBU MAOMBI**

**WITO WA KUITWA SHAURINI**

**KWA SPYTECH SECURITY SUPPLIES LTD**

**POPOTE MLIPO**

**Fahamu kwamba ALEXANDER KAFUPI GAUDENCE amefungua shauri katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya dhidi yako.**

**Shauri tajwa limepagwa kutajwa tarehe 05/10/2023 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mheshimiwa A.J. MALENGO Mwenyekiti wa Baraza.**

Hivyo unaamuliwa kuhudhuria wewe binafsi au mwakilishi wako anaeruhusiwa kisheria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa , ambapo nyalaka zote zihusuzo shauri hilo utazikuta kwenye masijala ya Baraza zilizopo mtaa wa Mahiwa, Kata ya Makorongoni barabara ya kwenda Pawaga mkabala na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Iringa.

Amri hii imetolewa na mkono wangu na mhuri wa Baraza leo hii tarehe 21/09/2023

A.J. MAJENGO
MWENYEKITI WA BARAZA.

DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL IRINGA TANZANIA

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI....................640 LA .2017**

**RAYMOND ERNEST SWAI................MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**MICHAEL SAMWEL KYANDE.....................MDAIWA/WADAIWA**
**FESTO MAHIMBA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**MICHAEL SAMWEL KYANDE**
**FESTO MAHIMBA**

**POPOTE ULIPO/MLIPO**

**RAYMOND ERNEST SWAI** Amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe ......09/10/2023 saa tatu Asubuhi mbele ya **Mh J.W. SILLAS** hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 22 mwezi 09..2023

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KISUTU**
**DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA MADAI NO.49 LA MWAKA 2023**

**CARLOS SLYIVESTER.......................................MDAI**

**DHIDI YA**

**TATA AFRICA HOLDINGS (T) LTD........................MDAIWA**
**DAR ES SALAAM.**

**Kuitwa shaurini**

Kwa kuwa mwombaji aliyetajwa hapo juu, ameleta shauri la maombi ya Madai dhidi yako; Maombi ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za maombi hayo zinazopatikana katika Mahakama hii, Hivyo basi unahitajika kuhudhuria katika Mahakama hii kupitia wakili au mwakilishi wako ambaye anaruhusiwa kisheria, siku ya tarehe 29/09/2023 saa tatu (3:00) kamili asubuhi mbele ya Mhe.RM RUBOROGA kujibu maombi haya dhidi yako.
Unaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo unatarajia kutumia kwaajili ya utetezi siku hiyo.
**ANGALIA:**
Kama usipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na mahakama hii ikithibitisha kuwa umepokea taarifa hii ya kuitwa shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wako.
HATI hii imetolewa kwa amri yangu na CHAPA ya Mahakama hii leo tarehe 27 septemba 2023.

MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI – KISUTU
DARESSALAAM

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KatikaMahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya GEITA**

**Kituo cha BULELA MKOA WA GEITA**

**Shauri la madai Na 25/2023**

**Jina la Mdai: ELIAS MWIHINJA**

**Jina la Mdaiwa: COSMAS MALULU**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuniya 18 ya kanun iza taratibu Madai katika mahakama za Mwanzo)**

**Kwa:COSMAS MALULU**
**WA DAR ES SALAAM**

**Kwa kuwaMdai ameleta madai yake YA TSH. 835,000/- (LAKI NANE NA ELFU THELATHINI NA TANO TU)**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii Tarehe 29 Mwezi 09 Mwaka 2023 saa2.00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta Shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:**Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini.Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 04 Mwezi 09 Mwaka 2023

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
BULELA_GEITA.

---

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0745 700 710.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Watu 100 wateketea kwa moto, akiwamo bibi na bwana harusi

**BAGHDAD,** Iraq

WATU 100 wamefariki dunia na wengine 150 kujeruhiwa baada ya jengo lililokuwa likitumika kwa sherehe ya harusi kuteketea kwa moto kaskazini mwa Iraq.

Mkurugenzi wa Afya, Ahmed Dubardan, alisema miongoni mwa watu waliofariki ni bwana na bibi harusi ambao walifunga ndoa muda mchache kabla ya tukio.

Akizungumza na wanahabari alisema watu 50 wako katika hali mbaya wanaendelea kupatiwa matibabu hospitalini baada ya kuungua na moto huo.

"Wengi wa waliojeruhiwa waliungua kwa asilimia kubwa kuanzia 50 hadi 60 ya miili yao. Hii si nzuri hata kidogo," alisema.

**Wengi wa waliojeruhiwa waliungua kwa asilimia kubwa kuanzia 50 hadi 60 ya miili yao. Hii si nzuri hata kidogo.**

Aliongeza kuwa idadi kubwa ya majeruhi ni vijana wa kiume na wa kike na hadi jana hakuna aliyeruhusiwa kuondoka hospitali.

Kulingana na taarifa hiyo, moto huo ulitokea juzi katika sherehe ya harusi iliyofanyika wilaya ya Al-Hamdaniya katika mkoa wa Nineveh kaskazini mwa Iraq.

Bado haijabainika kilichosababisha moto huo, lakini ripoti za mapema zilisema kuwa ulizuka baada ya fataki kuwashwa.

Picha iliyotumwa na shirika la habari la Iraq Nina, ilionyesha wazima moto wakipambana na moto huo, na picha kutoka kwa waandishi wa habari wa eneo hilo zilizochapishwa kwenye mitandao ya kijamii zinaonyesha mabaki ya nyumba iliyoteketea baada ya tukio hilo.

Walioshuhudia tukio hilo walisema mamia ya watu walikuwa ndani wakisherehekea wakati jengo lilipowaka moto saa nne na dakika 45 kwa saa za eneo hilo.

"Tuliona moto ukitokea nje ya ukumbi, waliofanikiwa walitoka na wengine walikwama waliungua moto. Hata waliotoka walionekana kuvunjika," alisema Imad Yohana. **BBC**



Wafanyakazi wa huduma ya dharula wakitafuta miili ya watu katika kifusi cha jengo kulikofanyika sherehe ya harusi na kuteketea kwa moto jana. **PICHA: REUTERS**

# Ufaransa yamuondoa balozi Niger

**NIAMEY,** Niger

BALOZI wa Ufaransa nchini Niger Sylvain Itte, hatimaye ameondoka nchini Niger jana baada ya kugoma kwa wiki kadhaa.

Hayo yameelezwa na vyanzo viwili vya usalama, ikiwa ni karibu mwezi mmoja tangu utawala wa kijeshi wa Niger kuamuru aondoke mara moja nchini humo.

Serikali ya kijeshi iliingia madarakani baada ya mapinduzi ya Julai 26 mwaka huu.

Agosti 25, serikali hiyo ilitoa amri kwa balozi huyo wa Ufaransa kuondoka nchini humo ndani ya saa 48, ikieleza hapaswi kuwa nchini humo kutokana na vitendo vya Ufaransa vilivyo kinyume na maslahi ya Niger.

Lakini agizo hilo hapo awali lilipuuzwa na Ufaransa, ambayo ilikataa kuwatambua viongozi hao wa kijeshi, na hivyo kusababisha maandamano ya kila siku mbele ya Ubalozi wa Ufaransa mjini Niamey.

Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron alibaini mwezi huu kwamba Balozi Itte na wasaidizi wake walikuwa wakishikiliwa kama mateka ndani ya ubalozi huo.

Mara kadhaa Macron alikuwa akisisitiza kwamba Ufaransa isingelibadilisha msimamo wake wa kuyalaani mapinduzi hayo ya kijeshi na kuahidi kumsaidia rais aliyepinduliwa, Mohamed Bazoum, kurudi madarakani.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Rais Macron alitangaza kuwa nchi yake imechukua uamuzi wa kuwaondoa wanajeshi wapatao 1,500 pamoja na Balozi wake nchini Niger. Katika mahojiano maalumu kupitia televisheni ya Ufaransa, pasipo kutoa ufafanuzi wa kina, alisikika akisema Ufaransa imeamua kumuondoa balozi wake na wafanyakazi wengine katika kipindi cha saa kadhaa. **DW**

# Kenya yatetea uamuzi wake kuwapeleka polisi Haiti

**NAIROBI,** Kenya

SERIKALI ya Kenya imesema ina uhakika kupelekwa kwa vikosi vya polisi wake nchini Haiti kutamaliza vita vya magenge ya kihalifu.

Kenya ina matumaini itakamilisha zoezi la kuwapeleka polisi wake katika nchi hiyo ifikapo Januari mwakani.

Mwaka jana serikali ya Haiti iliomba msaada kutoka jumuiya ya kimataifa kutokana na kuongezeka kwa ghasia za magenge ya kihalifu.

Magenge hayo kwa kiasi kikubwa yamewazidi nguvu polisi wa nchi hiyo na sasa yamedhibiti zaidi ya robo tatu ya mji mkuu.

Hapo awali maofisa wa Kenya walizungumza kuhusu askari 1,000 wanaokwenda Haiti kutoa mafunzo kwa polisi wa nchi hiyo na kusaidia kulinda mitambo muhimu.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Kenya Alfred Mutua, alisema kuwa kutakuwa na kikosi cha kuingilia kati kuwapokonya silaha wale aliowaita majambazi na magenge ya kihalifu.

Katika mahojiano na BBC Alfred Mutua alisema polisi wa Kenya watawaachilia raia wa Haiti ambao walitekwa nyara na kuwaachia huru wanawake waliokuwa wakibakwa.

Alisema hakutarajia kama kungekuwa na vurugu nyingi.

Baadhi walielezea mashaka kuhusu kupelekwa kwa vikosi vya polisi umbali wa kilomita 12,000 hadi nchini Haiti.

Wanaopinga suala hilo waliegemea changamoto nyingi za sheria na hali ya kukosa utulivu nchini Kenya.

Mashirika ya kutetea haki yamekuwa yakishutumu polisi wa nchi hiyo kwa kuhusishwa na vitendo vya ukatili ikiwa ni pamoja na mauaji na mateso. **BBC**

# Marekani yasitisha misaada Gabon

**WASHINGTON,** Marekani

MAREKANI imesitisha misaada yake kwa nchi ya Gabon kufuatia mapinduzi ya mwezi uliopita.

Katika taarifa ya waziri huyo, ilieleza hatua hiyo ya muda inaendana na hatua zilizochukuliwa na Jumuiya yakikanda ya Afrika ya Magharibi (Ecowas), Umoja wa Afrika (AU) na washirika wengine wa kimataifa kufuatia mapinduzi hayo.

Uanachama wa Gabon katika Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi na AU ulisitishwa kufuatia mapinduzi hayo. Ilisema uamuzi wa kusimamisha misaada kwa Gabon utabaki huku tukitathmini hali ya mambo nchini humo ukiendelea kufanyika.

Hata hivyo wizara hiyo ilisema kuwa inatambua shughuli nchini humo zinaendelea, ikiwa ni pamoja na shughuli za kidiplomasia na kibalozi kuwasaidia raia wa Marekani.

Tarehe 30 Agosti, viongozi wa kijeshi wa Gabon walimpindua Rais Ali Bongo baada tu ya kutangazwa mshindi katika uchaguzi mkuu.

Rais Bongo amekuwa madarakani tangu 2009. Alirithi kiti hicho kutoka kwa baba yake Omar Bongo, ambaye alikua rais kwa mara ya kwanza mwaka wa 1967. **BBC**

# YANGA YAIAMSHA NAMUNGO

Na Adam Fungamwango

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Cedric Kaze amesema mechi yao iliyopita dhidi ya Yanga imemuonyesha wazi sehemu ambazo wameimarika na zile zenye mapungufu.

**Kwa sasa anafanyia kazi maeneo ambayo ameona yana mapungufu kabla ya mchezo wao wa Jumamosi ijayo dhidi ya Mashujaa FC.**

Akizungumza na Nipashe akiwa mkoani Lindi, Kaze alisema tayari kikosi chake kimesharejea mazoezini kwenye uwanja wa Wonder Kids na wamekuwa wakifanyia kazi makosa yote yaliyoonekana na anaamini mchezo ujao watakuwa imara zaidi.

"Kikosi kinaendelea vizuri, kitu kizuri hatukupata majeraha katika mechi iliyopita ya ligi dhidi ya Yanga kuna vitu vizuri na kuna vingine siyo vizuri sana vimetokea na nimeviona katika mechi ile, sasa hivyo vyote tunavifanyia kazi, makosa yaliyojitokeza katika mechi ile tuliyachukua na sasa tumeanza kuyarekebisha na kuhakikisha tunapata pointi tatu muhimu kwenye mchezo wetu wa Septemba 30 dhidi ya Mashujaa," alisema Kaze.

Mechi iliyopita dhidi ya Yanga ilichezwa Septemba 20 Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, Namungo ilipoteza kwa bao 1-0 lililofungwa dakika tatu kabla mechi kumalizika na kiungo Mudathir Yahaya.

Timu hiyo haijashinda mechi yoyote ya Ligi Kuu tangu kuanza kwa msimu huu, ilipoteza kwa bao 1-0 dhidi ya JKT Tanzania, Agosti 15, sare ya bao 1-1 dhidi ya KMC Agosti 19 na ikafungwa bao 1-0 dhidi ya Yanga.

Kutokana na hali hiyo, nahodha msaidizi wa klabu hiyo Jacob Massawe amewatoa hofu mashabiki wa timu hiyo kuwa wataanza kufanya vyema katika mechi yao ijayo dhidi ya Mashujaa FC itakayopigwa Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi.

"Najua tuna deni kubwa kwa mashabiki wetu, tunaangalia jinsi gani tunaweza kuwafuta machozi kuelekea katika mechi yetu dhidi ya Mashujaa, najua siku nyingi wamemisi furaha," alisema Massawe ambaye ni mshambuliaji wa timu hiyo inayoshika nafasi ya 14 kwa sasa katika msimamo wa Ligi Kuu baada ya michezo mitatu kuchezwa.

BINJUKA...



Mchezaji wa mchezo wa Tenis, Ibrahim Kessy, akipiga mpira kurudisha kwa mpinzani wake (hayupo pichani), wakati alipokuwa akifanya mzoezi katika viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Tanzania Prisons wanaimani na Minziro*

Na Saada Akida

UONGOZI wa klabu ya Tanzania Prisons umesema unaimani na kocha wao Fred Felix 'Minziro' kuwafikisha katika malengo wanayoyatarajia kwa msimu huu wa 2023/24 wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kauli hiyo imekuja siku chache baada ya kuibuka tetesi kuwa uongozi huo umempa kocha huyo mechi tatu asipofanya vizuri kibarua chake cha kukinoa kikosi cha timu hiyo kitakuwa mashakani baada ya kutofanya vizuri kwenye mechi tatu za ligi hiyo walizocheza wakiambulia alama moja huku wakishika mkia kwenye msimamo.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa klabu hiyo, Enock Manguku alisema hakuna ukweli juu ya tuhuma hizo kwa sababu wanaimani na Minziro anaweza kuwafikisha kwenye malengo yao kwa msimu huu.

Alisema wanatambua ligi ni ngumu na ndio kwanza imeanza hivyo kupata alama moja kwenye michezo mitatu bado hakuwafanyi kumtimua kocha wao huyo.

"Pamoja kwa hatukuanza vizuri lakini bado hatuwezi kumpa mtihani kocha, tunaimani naye na ataendelea kukinoa kikosi chetu kwa sababu ni mapema sana na ligi ndio imeanza na timu inatengeneza muunganiko kwa wachezaji wapya na wale wa msimu uliopita," alisema Manguku.

Alisisitiza kuwa bado Minziro ataendelea kukinoa kikosi cha timu hiyo na kwa sasa anaendelea na maandalizi kwa ajili ya mechi zilizopo mbele yao ukiwemo mchezo unaofuata dhidi ya Simba.

Katika mchezo huo Tanzania Prisons watakuwa wenyeji wakiwakaribisha Simba, Oktoba 5, huku wakiwa na kibarua cha kusaka pointi tatu muhimu kwenye uwanja wa Sokoine, Mbeya.

## Nancy kufungua Tanzania Fashion Festival 2023

Na Frank Monyo

MREMBO wa Tanzania na 'Miss World Africa' mwaka 2005 Nancy Sumari anatarajiwa kuwa mgeni rasmi na kufungua Onesho la Mitindo la 'Tanzania Fashion Festival 2023' Septemba 30 mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana jijini Dar es Salaam, Mwanzilishi na mratibu wa onesho hilo, Deogratius Kithama, alisema kuwa huu ni mwaka wa sita tangu kuanzishwa kwa onesho hilo ambapo kwa mwaka huu wameandaa burudani kubwa na ya kuvutia kwa watu watakaoshiriki.

"Ni heshima kubwa kwetu kwa Nancy kukubali kufungua tamasha la mwaka huu kama mgeni rasmi, huku tukifahamu nguvu yake ya ushawishi kwenye mitindo na urembo Tanzania. Katika onesho la Jumamosi hii mbali na kuwa na maonesho ya mavazi, pia kutakuwa na burudani za muziki pamoja na dansi," alisema Kithama.

Alisema kuwa tamasha hilo ni nafasi muhimu kwa vijana wanaochipukia katika tasnia ya mitindo pamoja na wale waliopo kuja kuona mitindo mipya na kujifunza ili kuboresha kazi zao na kuweza kushiriki katika maonesho mbalimbali hata nje ya Tanzania.

## Mafunzo yaihofia Mlandege

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Mafunzo SC imesema mchezo wao dhidi ya Mlandege FC utakaochezwa kesho utakuwa mchezo mgumu na watatakiwa kupambana zaidi kupata alama tatu ili kufuta makosa yaliyofanyika katika michezo iliyopita.

Mafunzo SC ipo nafasi ya 10 katika msimamo wa Ligi ikiwa na alama mbili katika michezo mitatu aliyocheza ya Ligi Kuu ya Zanzibar.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha wa timu hiyo Abdalla Bakari "Edo" alisema hakuanza vizuri Ligi kuu ya Zanzibar hivyo matarajio makubwa ni kuona anapata alama tatu muhimu katika mchezo wake huo wa kesho.

Alisema katika michezo mitatu iliyopita licha ya kutengeneza nafasi, washambuliaji wake hawakuwa makini kuzitumia nafasi hizo lakini pia safu yao ya ulinzi haikuwa makini.

Aidha alisema kuwa msimu huu umekuwa mgumu zaidi kutokana na vilabu kufanya maandalizi mazuri na zote zinawania nafasi nne za juu.

Pia kocha Edo amewataka mashabiki wa Mfunzo FC kujitokeza kwa wingi kwenye Uwanja wa Mau kuwatia moyo wachezaji wao na kuwashangilia kwenye mchezo huo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### WATKINS AWANIWA

MKURUGENZI wa michezo wa Arsenal, Edu amefanya mazungumzo na wakala mshambuliaji wa Aston Villa, Ollie Watkins kuhusu uhamisho wa mchezaji huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 27, huku Chelsea pia ikimtaka mchezaji huyo. ***(Football Transfers)***

### ....VILLA WAKOMAA

HATA hivyo klabu ya Aston Villa imesalia kwenye mazungumzo kuhusu kuongeza mkataba wa Watkins na wanataka mkataba mpya ukamilishwe ifikapo Januari. ***(90 min)***

### TONEY AWANIWA

KLABU za Arsenal na Chelsea ziko tayari kutoa wachezaji pamoja na fedha katika majaribio yao ya kumsajili mshambuliaji wa England, Ivan Toney kutoka Brentford, ambaye kuna uwezekano wa kutaka zaidi ya pauni milioni 75 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27. ***(90 min)***

### LONGSTAFF MKATABA MPYA

KLABU ya Newcastle United inatazamiwa kuanza mazungumzo na kiungo wa kati wa Brazil, Joelinton mwenye umri wa miaka 27, na kiungo wa kati wa England, Sean Longstaff mwenye umri wa miaka 25, kuhusu kuongeza mikataba yao, ambayo yote inatazamiwa kumalizika Juni 2025. ***(Football Insider)***

### NDIDI ATAKIWA

KLABU ya Barcelona inafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Nigeria, Wilfred Ndidi mwenye umri wa miaka 26, wakati mkataba wake na Leicester City utakapokamilika mwishoni mwa msimu huu. ***(Sport)***

### GALTIER AFUATILIWA

NAPOLI inamfuatilia kocha wa zamani wa Paris St-Germain, Christophe Galtier kufuatia mwanzo mbaya wa msimu chini ya Rudi Garcia, wakati Marseille pia wanavutiwa na mchezaji wao huyo wa zamani. ***(RMC Sport)***

### RATCLIFFE AITAKA MAN

BILIONEA wa England, Sir Jim Ratcliffe yuko tayari kurekebisha ofa yake ya kuinunua Manchester United na yuko kwenye makubaliano na wamiliki wa sasa wa Glazers. (Mirror)

### CANCELO NA BARCA

BARCELONA imekubali kwa mdomo ada ya euro milioni 35 na Manchester City kubadilisha mkopo wa beki wa pembeni wa Ureno, Joao Cancelo kuwa mkataba wa kudumu. ***(El Chiringuito TV)***

### SESKO NA MAN

MSHAMBULIAJI wa Slovenia, Benjamin Sesko mwenye umri wa miaka 20 amesema alizungumza na Manchester United msimu uliopita kabla ya kuondoka Red Bull Salzburg, lakini alihisi kuhamia RB Leipzig kulikuwa bora ili kujiimarisha. ***(Transfermarkt)***

### YOUNG ANYATIWA MAN

KLABU ya Manchester City imeelekeza macho yake kwa mlinda mlango wa Sunderland, Matty Young mwenye umri wa miaka 16. ***(Mail)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SAKA AIPA PIGO ARSENAL

**LONDON,** England

BUKAYO Saka wa Arsenal amejiunga na orodha ya wachezaji majeruhi inayoongezeka kwenye klabu hiyo na kuna shaka kama ataweza kucheza mechi zao mbili zijazo, kocha Mikel Arteta amesema.

**Mshambuliaji huyo wa England Saka aliumia katika sare ya 2-2 nyumbani na Tottenham Hotspur siku ya Jumapili ambapo alifunga na kufikisha mechi yake ya 86 kwenye Ligi Kuu kwa Arsenal.**

Alipoulizwa kama Saka anaweza kukosa mechi zijazo, Arteta aliwaambia waandishi wa habari: "Inawezekana.

"Alikuwa akichechemea baada ya mchezo dhidi ya Spurs, ambayo kamwe si dalili nzuri. Hajaweza kushiriki katika kipindi cha mazoezi."

Arteta alisema kiungo wa kati Declan Rice pia hajafanya mazoezi tangu alipotolewa katika kipindi cha mapumziko kwenye mchezo wa dabi ya London kaskazini kwa matatizo ya misuli, akiongeza: "Hangeweza kuendelea na mchezo na tunatumaini sio tatizo kubwa sana.

"Tunajiamini. Hakuwa na raha na hiyo haikuwa dalili nzuri. Tunatumaini atakuwa bora."

Raia huyo wa Hispania aliongeza kuwa Leandro Trossard, Gabriel Martinelli na Thomas Partey bado majeruhi.

"Ni orodha ndefu ... Ni hali tuliyo nayo kwa sasa na tunahitaji wachezaji warudi, hilo ni la uhakika," alisema Arteta.

●●● Mshambuliaji huyo aliumia kwenye dhidi ya Spurs na sasa kuna shaka kuikosa....

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,157,2

MECHI KALI
OSASUNA
VERSUS
ATLETICO MADRID
1 | 3.25
X | 3.30
2 | 2.27

tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!
1. Saidi Saidi - 0656855902
2. Masanja Maduhu - 0673 089 XXX
3. Yona Julius - 0712 000 XXX
4. Eliana Isaya - 0714 250 XXX
5. Badru Said - 0715 305 XXX
6. Balaka Danyeli - 0717 756 XXX
7. Issack Javan - 0718 386 XXX
8. Haji Mnavi - 0719 081 XXX
9. Revocatus Kaijage - 0719 383 XXX
10. Chum Haji Chum - 0779 335 XXX
20,000/= KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# TEN HAG ATAKA ZAIDI KUTOKA KWA GARNACHO

**MANCHESTER,** Uingereza

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag amefichua kwamba Alejandro Garnacho aliondolewa baada ya mechi mbili za kwanza za msimu huu kwa sababu uchezaji wake "haukuwa mzuri vya kutosha."

Garnacho alianza dhidi ya Wolves na Tottenham Hotspur Agosti, lakini aliachwa nje ya timu kwa mechi tano kabla ya kurejea na bao katika ushindi wa 3-0 dhidi ya Crystal Palace Jumanne. Lilikuwa bao la kwanza kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 msimu huu na Ten Hag amemtaka fowadi huyo kuendelea kuimarika.

"Umeona mwanzoni mwa msimu tulimchezesha, mchango wake haukuwa mzuri," alisema Ten Hag.

"Unaona siku zote ni tishio kwenye mchezo hata asipocheza vizuri, anatakiwa kujifunza anapofanya kazi yake, atakuwa na wakati wake na atakuwa na maamuzi kwa sababu ana sifa kubwa. .

"Nataka kuona kama leo (juzi), anaingia kwenye kisanduku mahali pazuri kumaliza.

"Nadhani ni kawaida kabisa kwa mchezaji wa umri wake kuwa kuna nafasi ya kuimarika sana, kila mtu anampenda, mashabiki wanampenda, timu inampenda, mimi nampenda, lakini pia lazima tudai kutoka kwake."

Pamoja na Garnacho, Ten Hag pia aliwaanzisha Mason Mount, Raphaël Varane na Harry Maguire huku United ikijikatia tiketi katika raundi ya nne ya Kombe la Carabao.



# Guardiola: Phillips atamrithi Rodr

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amethibitisha kuwa Kalvin Phillips atapata nafasi ya kuichezea Manchester City baada ya Rodri aliyefungiwa.

Rodri atakosa mechi tatu zijazo za nyumbani baada ya kuoneshwa kadi nyekundu ya moja kwa moja katika ushindi wa hivi majuzi wa City dhidi ya Nottingham Forest, na kufungua milango kwa Phillips kuanza. Tangu ajiunge kutoka Leeds United msimu wa joto wa 2022, Phillips amecheza dakika 645 tu katika mashindano yote, na mechi nne tu kati ya 24 alizoanza.

Hata hivyo, huku Rodri akitarajiwa kukosa mechi tatu zijazo za nyumbani, Phillips anatazamiwa kuchukua nafasi yake kwenye safu ya kiungo ya City, akianza na mechi ya raundi ya tatu ya Kombe la Carabao jana Jumatano dhidi ya Newcastle United.

"Kalvin ataanza," alisema Guardiola akithibitisha katika mkutano na waandishi wa habari Jumanne.

Guardiola aliendelea: "Sio wiki hii tu kwa mara nyingi, mara nyingi tangu awasili, amekuwa muhimu sana.

"Uthabiti wake, anafanya kila kitu katika mchezo kile kilichotokea dhidi ya Nottingham, ilikuwa ni ulinzi zaidi, ustahimilivu, ulinzi na alitusaidi pumua.

"Kitu muhimu ni w unachukua hatua katika r ndogo tunajaribu kumsaidi

Nafasi ndogo ya Phillips k klabu ya City ilimfanya a sana uhamisho wakati wa sha la majira ya joto, huku pool na Bayern Munich wa miongoni mwa klabu zilizo zinamuwania.

Kiungo huyo wa kati ali wazi mapema msimu wa kwamba hataki kuondok baada ya kutokuwa na uh juu ya mustakabali wake, hatimaye iliamua kumba mchezaji huyo mwenye um miaka 27.

## HABARI MICHEZO


# 90,273/-

## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 30/09/23 | 19:30 | Tottenham Hotspur vs Liverpool FC | 2.80 | 3.90 | 2.15 |
| 02. 30/09/23 | 20:00 | Boavista Porto vs FC Famalicao | 2.17 | 3.30 | 3.15 |
| 03. 30/09/23 | 22:00 | Real Sociedad San Sebastian vs Athletic Bilbao | 2.21 | 3.15 | 3.25 |
| 04. 30/09/23 | 22:00 | AS Monaco vs Olympique Marseille | 2.20 | 3.65 | 2.85 |
| 05. 01/10/23 | 13:30 | Fatih Karagumruk Istanbul vs Kasimpasa Istanbul | 2.28 | 3.35 | 2.60 |
| 06. 01/10/23 | 14:30 | FC Nuremberg vs FC Magdeburg | 2.37 | 3.55 | 2.65 |
| 07. 01/10/23 | 14:30 | SV 07 Elversberg vs Greuther Furth | 2.50 | 3.60 | 2.48 |
| 08. 01/10/23 | 14:30 | VfL 1899 Osnabruck vs FC Kaiserslautern | 2.65 | 3.45 | 2.42 |
| 09. 01/10/23 | 16:00 | Nottingham Forest vs Brentford FC | 2.70 | 3.15 | 2.55 |
| 10. 01/10/23 | 16:00 | Udinese Calcio vs Genoa CFC | 2.08 | 3.20 | 3.45 |
| 11. 01/10/23 | 17:15 | Deportivo Alaves vs CA Osasuna | 2.55 | 3.00 | 2.80 |
| 12. 01/10/23 | 17:30 | FC Luzern vs FC Zurich | 2.24 | 3.25 | 2.70 |
| 13. 01/10/23 | 18:00 | FK Austria Wien vs SK Rapid Wien | 2.33 | 3.35 | 2.55 |
| 14. 01/10/23 | 18:00 | Hobro IK vs Kolding IF | 2.65 | 3.25 | 2.31 |
| 15. 01/10/23 | 19:00 | Konyaspor vs Besiktas Istanbul | 2.80 | 3.30 | 2.19 |
| 16. 01/10/23 | 19:00 | Viborg FF vs AGF Aarhus | 2.60 | 3.35 | 2.50 |
| 17. 01/10/23 | 19:00 | Atalanta BC vs Juventus Turin | 2.46 | 3.30 | 2.70 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 28/09/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 2922 | Urartu vs Bkma Yerevan | 1.50 | 3.98 | 5.51 |
| 16:00 | 3694 | Al Masry Club vs Farco FC | 1.97 | 3.10 | 3.94 |
| 16:20 | 4006 | Hatta Club vs Al Nasr Dubai | 3.54 | 3.80 | 1.77 |
| 16:30 | 1281 | AL Ansar vs AL Ahed | 3.10 | 3.30 | 2.02 |
| 17:00 | 2115 | FC Nomme United vs Viimsi JK | 1.64 | 4.41 | 4.30 |
| 17:00 | 2619 | Pakhtakor vs Otmk Olmaliq | 1.56 | 3.75 | 4.96 |
| 17:00 | 5918 | FC Elva vs Paide Linnameeskond | 2.33 | 3.93 | 2.59 |
| 17:30 | 2000 | Panserraikos vs PAS Giannina | 2.18 | 3.12 | 3.38 |
| 17:30 | 5632 | Delhi Dynamos FC vs Mumbai City FC | 3.18 | 3.58 | 1.94 |
| 18:30 | 4701 | Maribor vs NK Radomlje | 1.33 | 4.76 | 6.88 |
| 19:00 | 1902 | Najma Manama vs Al Shabbab | 2.36 | 2.96 | 2.96 |
| 19:00 | 2677 | JK Welco Elekter vs Viljandi Tulevik | 1.91 | 4.03 | 3.06 |
| 19:00 | 2680 | Ismaily SC vs El Ittihad Alexandria | 2.42 | 3.03 | 2.93 |
| 19:00 | 2839 | GKS Tychy vs Wisla Plock | 2.75 | 3.11 | 2.41 |
| 19:00 | 3132 | Al Sharjah SC vs Al Ain | 2.82 | 3.53 | 2.12 |
| 19:00 | 3648 | Manama Club vs Al Hala Muharraq | 1.58 | 3.51 | 5.50 |
| 19:15 | 4086 | KA Akureyri vs Vestmannaeyjar | 2.06 | 3.62 | 2.96 |
| 19:30 | 1610 | Frosinone vs Fiorentina | 3.70 | 3.65 | 1.98 |
| 19:30 | 3066 | Monza vs Bologna | 2.43 | 3.35 | 2.94 |
| 19:30 | 4282 | Racing White Daring Molenbeek vs Union Saint Gilloise | 4.58 | 3.88 | 1.64 |
| 20:00 | 1232 | Orebro SK vs Utsiktens BK | 2.17 | 3.34 | 3.23 |
| 20:00 | 1602 | GIF Sundsvall vs Gefle IF | 1.78 | 3.72 | 4.19 |
| 20:00 | 1762 | AL Markhiya vs Lekhwiya SC | 7.87 | 5.25 | 1.26 |
| 20:00 | 2415 | Trelleborgs FF vs Jonkopings Sodra | 2.01 | 3.55 | 3.45 |
| 20:00 | 2628 | Kotwica Kolobrzeg vs Nieciecza KS | 3.10 | 3.10 | 2.20 |
| 20:00 | 2633 | Ida-Virumaa FC Alliance vs FC Tallinn | 6.68 | 5.64 | 1.35 |
| 20:00 | 2719 | Al Arabi Doha SC vs Qatar SC | 1.86 | 3.54 | 3.44 |
| 20:00 | 3864 | Orgryte IS vs Gais | 3.60 | 3.60 | 1.94 |
| 20:00 | 4499 | Celta Vigo vs Alaves | 1.78 | 3.40 | 5.12 |
| 20:00 | 5081 | Valerenga vs Bodo Glimt | 3.05 | 3.72 | 1.99 |
| 20:00 | 5650 | Fenerbahce vs Basaksehir | 1.48 | 4.17 | 5.82 |
| 20:00 | 5983 | Granada vs Betis | 2.93 | 3.39 | 2.42 |
| 20:30 | 1313 | Asteras Tripolis vs Panathinaikos | 6.25 | 3.38 | 1.61 |
| 21:00 | 4136 | AZ Alkmaar vs Heracles Almelo | 1.26 | 5.55 | 8.72 |
| 21:00 | 4531 | Lech Poznan vs Rakow Czestochowa | 2.17 | 3.18 | 2.98 |
| 21:00 | 5124 | AEK Athens vs Atromitos | 1.18 | 6.22 | 14.52 |
| 21:15 | 1202 | Olimpija Ljubljana vs Luka Koper | 1.77 | 3.57 | 3.77 |
| 21:30 | 1836 | FC Stade LS Ouchy vs Yverdon-Sport FC | 2.16 | 3.62 | 2.89 |
| 21:30 | 5490 | FC Basel vs FC Luzern | 2.47 | 3.51 | 2.53 |
| 21:45 | 2218 | Brugge vs Racing Genk | 1.77 | 3.74 | 3.94 |
| 21:45 | 4870 | Genoa vs Roma | 3.66 | 3.10 | 2.20 |
| 22:00 | 4488 | Wisla Krakow vs Lechia Gdansk | 1.85 | 3.41 | 3.77 |
| 22:15 | 1248 | Casa Pia Atletico vs Nacional Madeira | 1.65 | 3.71 | 5.12 |
| 22:15 | 2558 | CF Estrela vs Sporting Braga | 4.39 | 3.79 | 1.69 |
| 22:15 | 3292 | Vikingur Reykjavik vs Hafnarfjordur | 1.61 | 4.06 | 4.26 |
| 22:15 | 3747 | Valur vs Breidablik | 2.19 | 3.67 | 2.70 |
| 22:15 | 4032 | Stjarnan vs KR Reykjavik | 2.02 | 3.66 | 3.00 |
| 22:15 | 4902 | Fram Reykjavik vs Keflavik IF | 1.84 | 3.73 | 3.47 |
| 22:15 | 5501 | HK Kopavogs vs Fylkir | 2.21 | 3.71 | 2.65 |
| 22:30 | 1929 | Osasuna vs Atletico Madrid | 3.25 | 3.30 | 2.27 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.




# JKT TANZANIA YATAMBA KUIPA KICHAPO CHA 'KK' KAGERA SUGAR

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KLABU ya JKT-Tanzania imetamba kuishushia Kagera Sugar kichapo cha kizalendo 'KK' katika mchezo wao wa kesho wa ligi kuu Tanzania Bara kwenye uwanja wa CCM Kambarage mkoani hapa.

Akizungumza na Waandishi wa habari jana, Ofisa Habari wa JKT-Tanzania, Masau Bwire, alisema timu yake imejiandaa vizuri na mchezo huo ambao ni muhimu kwao na wamewaandalia kipigo hicho cha kizalendo.

**Alisema JKT Tanzania imeuchagua Uwanja wa CCM Kambarage Mjini Shinyanga kama Uwanja wao wa nyumbani katika msimu mzima wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya uwanja wao wa nyumbani kufungwa kupisha ukarabati mkubwa.**

"Tunatoa wito kwa Mashabiki wa JKT-Tanzania wasikate tamaa katika Michezo yetu miwili iliyopita ambayo tulipoteza dhidi ya Yanga na KMC ambayo tulikuwa hatujajipanga vizuri,lakini kwa sasa tupo vizuri, tumeshajitafuta na tutalionyesha hili kwenye mchezo wetu wa Ijumaa (kesho)" alisema Bwire.

Aidha, alisema wachezaji wao wako vizuri kiafya na hakuna majeruhi, wamejipanga kufanya vyema katika mechi zao zote zijazo na watamaliza msimu wa ligi kuu katika nafasi nzuri.

"Niwaambie watanzania, JKT Tanzania sasa tumejipata, mchezo wetu dhidi ya Kagera Sugar tutaanza kuwaonyesha mashabiki nini tunakitaka msimu huu, tunataka kuhakikisha tunamaliza ligi tukiwa kwenye nafasi za juu zaidi," alisema Bwire

Alitoa wito kwa wakazi wa Shinyanga wawaunge mkono kama timu yao ya nyumbani, na wajitokeze kwa wingi kuwashangilia ili kuwapatia nguvu na hamasa.



Msemaji wa Klabu ya JKT Tanzania, Masau Bwire, akizungumza na waandishi wa habari juu ya mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar kesho. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Gamondi aimarisha pumzi Yanga

INATOKA UK. 24

ni wachezaji na benchi lao la ufundi kuhakikisha wanafuzu hatua hiyo kwa mara ya kwanza baada ya miaka 24.

"Wachezaji na benchi la ufundi wote wanajua nini mashabiki wa yanga wanataka, na ndio maana unaona kocha anawapa mbinu tofauti tofauti wachezaji ili kuhakikisha tunafuzu hatua ya makundi ya michuano hii," alisema Harrison.

Yanga inahitaji sare au ushindi wowote kufuzu hatua hiyo ya makundi kufuatia ushindi wa mabao 2-0 walioupata kwenye mchezo wa kwanza uliochezwa Kigali, Rwanda.

Wakati Yanga wakisema hivyo, wawakilishi wengine wa Tanzania kwenye michuano hiyo, Simba wenyewe wameweka wazi kuwa mchezo wao wa Jumapili dhidi ya Power Dynamos utakuwa sehemu ya maandalizi yao ya kushiriki michuano ya 'Africa Football League, AFL, yanayotarajiwa kufanyika mwezi ujao.

Kocha Roberto Oliviera 'Robertinho' alisema mchezo wao wa marudiano Jumapili ijayo licha ya kusaka tiketi ya kutinga hatua ya makundi lakini watautumia kama sehemu yao ya maandalizi kuelekea kwenye mchezo wao wa ufunguzi wa michuano ya AFL dhidi ya Al Ahly.

## *Tanzania rasmi mwenyeji*

INATOKA UKURASA 24

viwanja," alisema.

Msigwa pia alisema si upande wa michezo tu utakaofaidika na kunufaika na uwenyeji wa fainali hizo, bali kwenye sekta nyingine mbalimbali kama Utalii, Biashara, Usafirishaji, Vyakula kutokana na kupokea wenyeji wengi watakaokuja kucheza, kuchezesha, kuangalia, kuripoti, kushabikia timu zao kutoka nchi mbalimbali za Afrika na Dunia kwa ujumla.

Hivi karibuni kabla ya kuelekea jijini Cairo kulikuwa na kikao kizito kilichofanyika jijini Dar es Salaam cha Makatibu Wakuu wa Wizara husika kutoka nchi zote tatu, Wenyeviti wa Mabaraza ya Michezo, Maofisa Watendaji Wakuu lengo ni kuandaa mikakati ya kuhakikisha jambo hilo linafanikiwa.

Vikao hivyo vilihitimishwa na Mawaziri wa nchi hizo ambao baada ya hapo walihamishia nguvu zao nchini Misri kwenye Mkutano wa CAF wa kutangaza wenyeji wa fainali hizo.

Wakati wa kutangazwa jijini Cairo, ujumbe wa Watanzania uliongozwa na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk Damas Ndumbaro, Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), Wallace Karia, Makamu wake Athumani Nyamlani na Mkurugenzi wa Sheria, Habari na Masoko TFF, Boniface Wambura.

Katika mkutano huo, CAF iliitangaza pia nchi ya Morocco kuwa mwenyeji wa fainali hizo za mwaka 2025.

# Michezo

Alhamisi Septemba 28, 2023

Nipashe




Ten Hag ataka zaidi kwa Garnacho UKURASA 22




Rais wa Shirikisho la soka Afrika (CAF) Patrice Motsepe akiwa ameshika karatasi maalum inayozionyesha nchi za Kenya, Uganda na Tanzania kuwa wenyeji wa Fainali za Afcon mwaka 2027 baada ya kutangazwa rasmi jana jijini Cairo, Misri. **PICHA: MTANDAO**

# *Tanzania rasmi mwenyeji AFCON 2027*

## ●●● Serikali yafurahishwa, kuanza ujenzi viwanja viwili Dodoma, Arusha, kukarabati vingine.....

**Na Adam Fungamwango**

TANZANIA kwa kushirikiana na nchi za Kenya na Uganda imefanikiwa kupata nafasi ya kuwa wenyeji wa Fainali za Mataifa ya Afrika za 2027.

**Nchi hizo za Afrika Mashariki zimepata nafasi ya kuandaa fainali hizo kwa pamoja baada ya kushinda maombi yao katika kura zilizopigwa jana jijini Cairo nchini Misri na kuzishinda nchi za Misri, Senegal na Namibia.**

Baada ya kampeni kabambe zilizofanywa na nchi mbalimbali zilizoomba, hatimaye Shirikisho la Soka Afrika (CAF), likatangaza rasmi kuwa mwaka 2027 Tanzania itakuwa mwenyeji wa fainali hizo kwa kushirikiana na nchi za Kenya na Uganda.

Hii ni mara ya kwanza kwenye historia ya nchi hizo tangu zipate uhuru kuandaa michuano hiyo mikubwa barani Afrika kwa ngazi za timu za taifa.

Mara baada ya CAF kuzipa rasmi uwenyeji nchi hizo, Serikali ya Tanzania imesema imefurahishwa mno kupata nafasi hiyo adhimu na ni furaha na heshima kubwa kwa nchi.

Akizungumza na gazeti hili jana muda mfupi baada ya CAF kuzitangaza nchi hizo za Afrika Mashariki, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa alisema baada ya kufanikiwa kupata nafasi hiyo, kinachofuata sasa ni kutengeneza miundombinu kwa kujenga viwanja vipya viwili katika miji ya Dodoma na Arusha na kukarabati vingine saba.

Aidha, Msigwa alipeleka pongezi zake kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan kwa kukubali kufanyika kwa mchakato huo wa Tanzania kuwa mwenyeji wa fainali hizo.

"Kwanza kabisa tumpongeze Rais kwa sababu ndiye aliyekubali mchakato huu wa maombi ufanyike, na amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha miundombinu inafanyiwa kazi mapema ili kuweza kufanikisha jambo hilo, ndiyo maana unaona mpaka sasa kuna ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa utakaogharimu Sh Bilioni 31, na pia kutajengwa viwanja viwili Dodoma na Arusha ambavyo vitatumika kwenye fainali hizo," alisema Msigwa.

Alisema kwa sasa wanaanza maandalizi kabambe katika nyanja mbalimbali ili hata fainali hizo zikimalizika wageni wote waliokuja wawe na hamu tena ya kutembelea Tanzania, lakini pia kutengeneza mazingira mazuri ya kuwa tayari kuomba tena uwenyeji mwingine kwa miaka ya mbele.

"Kwa sasa tupo kwenye maandalizi ya African Football League ambapo Simba wanaiwakilisha nchi na watacheza dhidi ya Al Ahly ya Misri kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa ambao uko kwenye ukarabati, lakini pia tuna ule mkakati wa kukarabati viwanja saba kama tulivyowahi kuahidi huko nyuma, hiyo yote ni upande wa miundombinu ya

INAENDELEA UKURASA 23

# Gamondi aimarisha pumzi Yanga, Robertinho kuwatumia Dynamos AFL

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

KUELEKEA kwenye michezo ya marudiano ya kufuzu hatua ya makundi ya Ligi ya mabingwa Afrika, klabu za Simba na Yanga zimeweka mikakati yake kuhakikisha wanafuzu kwa hatua hiyo.

Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi katika kuhakikisha anapata ushindi kwenye mchezo wao dhidi ya Al Merrikh Jumamosi ijayo ameonekana kuwaongezea dozi ya mazoezi wachezaji wake ambapo jana alionekana akiwakimbiza wachezaji wake kwa kasi mazoezini, wakizunguka uwanja.

Aidha, Gamondi alionekana kuwafanyisha mazoezi ya nguvu akilenga kuwaongezea stamina na kasi kuelekea kwenye mchezo huo utakaochezwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya jiji la Dar es salaam.

Akizungumza na gazeti hili, Gamondi, alisema anataka kona wanacheza kwa kasi muda wote na kutowapa nafasi wapinzani wao.

"Tulikuwa na mfumo mwingine kwenye mchezo wetu wa kwanza wa ugenini, na mchezo wa marudiano pia tutakuwa na mfumo mwingine kabisa, mazoezi ninayowafanyisha wachezaji wangu ni katika kuhakikisha kikosi kinakuwa imara na tunafikia malengo yetu, nataka kucheza soka la kasi zaidi," alisema Gamondi.

Alisema anataka kuona kila mchezaji anatimiza majukumu yake na timu kutumia vyema kila nafasi watakayoipata.

Kwa upande wake Menaja wa timu hiyo, Walter Harrison alisema maandalizi yote kuelekea kwenye mchezo huo muhimu yamekamilika kwa kiasi kikubwa na kazi iliyobaki

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >